# MCHANGO WA MANDHARI KATIKA KUFANIKISHA UJUMBE KATIKA RIWAYA *ROSA MISTIKA* NA *MAISHA KITENDAWILI*

**SHADRACK TETE MUIA**

**C50-7325-2016**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA ISIMU NA LUGHA CHUO KIKUU CHA MACHAKOS.**

**MACHI, 2023**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe wala haijawasilishwa kwa utathimi wa shahada ya uzamili katika chuo chochote kingine.

Sahihi.................................... Tarehe.................................... 17/03/2023

Shadrack Tete Muia

C50-7325-2016

**IDHINI YA WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Machakos.

Sahihi.................................... Tarehe.................................... 20/3/2023

Dkt. Makoti Vifu Saidi

Idara ya Isimu na Lugha

Chuo Kikuu cha Machakos

Sahihi.................................... Tarehe.................................... 20/3/2023

Dkt. Mutua John

Idara ya Isimu na Lugha

Chuo Kikuu cha Machakos

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi, mke wangu mpendwa Loise Mutua na watoto wangu wapendwa Ndanu Tete, Pendo Tete na Amani Muuo. Asanteni sana kwa uvumilivu wenu na kunitia moyo katika masomo yangu.

# SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uhai, afya na uwezo ulioniwezesha kukamilisha kazi hii. Nawashukuru pia wasimamizi wangu, Dkt. John Mutua na Dkt. Makoti V. Saidi kwa kutenga muda wao kupitia kazi yangu na kunielekeza vilivyo. Maarifa yao, mapendekezo ya kitaalam pamoja na mawaidha ya kiusomi waliyonipa ndiyo yamefanikisha kazi hii. Aidha, nawashukuru wahadhiri wengine wa Chuo Kikuu cha Machakos, hasa wa Idara ya Isimu na Lugha walionifunza, kunielekeza na kunitia moyo hadi kukamilisha kuandika tasnifu hii. Nao ni Dkt.Larry Ndivo na Dkt. Charles Kebaya.Shukrani za dhati ziwaendee wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika masomo ya shahada ya uzamili. Hawa ni Dorcas, Virginia, Angela, Agnes na wengineo. Pia, nashukuru familia yangu kwa kunivumilia, kunitia moyo na kuniombea nilipokuwa naendelea na masomo yangu. Mwisho, natoa shukrani za dhati kwa wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kufanikisha tasnifu hii.

**YALIYOMO**

UNGAMO .......... ii
TABARUKU .......... iii
SHUKRANI .......... iv
YALIYOMO .......... v
IKISIRI .......... viii
ABSTRACT .......... ix
SURA YA KWANZA .......... 1
1.0 Utangulizi .......... 1
1.1 Usuli wa Mada .......... 1
1.2 Suala la Utafiti .......... 3
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 4
1.4 Maswali ya Utafiti .......... 4
1.5 Sababu za kuteua Mada .......... 4
1.6 Upeo na mipaka ya Utafiti .......... 6
1.7 Msingi wa Kinadharia .......... 6
1.7.1 Nadharia ya Uhalisia .......... 7
1.7.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia .......... 10
SURA YA PILI .......... 11
YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI .......... 11
2.0 Utangulizi .......... 11
2.1 Vitabu .......... 11
2.2 Tasnifu .......... 14
SURA YA TATU .......... 18
MBINU ZA UTAFITI .......... 18
3.0 Utangulizi .......... 18
3.1 Ukusanyaji wa Data .......... 18
3.2 Usampuli .......... 18
3.3 Vifaa vya Utafiti .......... 19
3.4 Uchanganuzi wa Data .......... 19

3.5 Uwasilishaji wa Data ........ 20
SURA YA NNE ........ 21
UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ........ 21
4.0 Utangulizi ........ 21
4.1 MANDHARI YALIVYOSAWIRIWA KATIKA *MAISHA KITENDAWILI* ........ 21
4.1.1 Mandhari ya mahali ........ 22
4.1.1.1 Mandhari ya Nyumbani ........ 22
4.1.1.2 Mandhari ya Chuoni ........ 26
4.1.1.3 Mandhari ya Kanisani ........ 28
4.1.1.4 Mandhari ya Hospitalini ........ 30
4.1.1.5 Mandhari ya Ugangani ........ 31
4.1.1.6 Mandhari ya Mjini ........ 32
4.1.2.0 Mandhari ya Hali ........ 34
4.1.2.1 Mandhari ya Mazishini ........ 34
4.1.2.2 Mandhari ya Afya ........ 35
4.2 MANDHARI YALIVYOSAWIRIWA KATIKA *ROSA MISTIKA* ........ 37
4.2.0 Utangulizi ........ 37
4.2.1Mandhari ya Mahali ........ 37
4.2.1.1 Mandhari ya Nyumbani ........ 37
4.2.1.2 Mandhari ya Shuleni ........ 39
4.2.1.3 Mandhari ya Baa ........ 42
4.2.1.4 Mandhari ya Mjini ........ 43
4.2.3.0 Mandhari ya Wakati ........ 44
4.2.3.1 Mandhari ya Usiku ........ 44
4.2.4 Mandhari ya Hali ........ 46
4.2.4.1 Mandhari ya Huzuni ........ 46
4.3 MCHANGO WA MANDHARI KATIKA KUWASILISHA UJUMBE ........ 47
4.3.1 Utangulizi ........ 47
4.3.2 Ujumbe katika riwaya *Maisha Kitendawili* ........ 48
4.3.2.1 Utabaka ........ 48
4.3.2. 2 Ujumbe wa Dhuluma ........ 54

4.3.2.3 Kudumisha Utamaduni ....................................................................................57
4.3.2.4 Uvumilivu katika Ndoa.....................................................................................60
4.4.0 Ujumbe katika riwaya ya Rosa Mistika ..............................................................63
4.4.1 Utangulizi..........................................................................................................63
4.4.2 Uvumilivu katika Ndoa.......................................................................................64
4.4.3 Nafasi ya Mwanamke katika jamii .....................................................................66
4.4.4 Ujumbe wa Dhuluma .........................................................................................69
4.4.5 Utamaduni.........................................................................................................71
4.4.6 Utabaka .............................................................................................................73
4.5 UHALISIA WA MANDHARI...................................................................................75
4.5.1 Utangulizi..........................................................................................................75
4.5.2 Uhalisia katika riwaya Maisha Kitendawili na Rosa Mistika ................................76
4.6 Hitimisho...............................................................................................................82
SURA YA TANO ........................................................................................................87
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..............................................................................87
5.0 Utangulizi..............................................................................................................87
5.1 Matokeo ya Utafiti .................................................................................................87
5. 2 Hitimisho..............................................................................................................89
5.3 Mchango wa Utafiti ...............................................................................................90
5.4 Mapendekezo ........................................................................................................90
MAREJELEO ............................................................................................................91
KIAMBATISHO I ........................................................................................................94
KIAMBATISHO II .......................................................................................................95

# IKISIRI

Lengo la kila mwandishi wa kazi ya fasihi ni kufikisha ujumbe kwa msomaji. Ili kuwasilisha ujumbe huo kikamilifu, inambidi mwandishi atumie mbinu za kisanii mbalimbali. Mbinu za kisanii hujumuisha jinsi masimulizi hufanywa kupitia kwa wahusika, mbinu za uandishi, mandhari na lugha. Mandhari ni mojawapo ya kipengele cha mbinu za kisanii ambacho hudokeza mahali matukio ya hadithi au masimulizi hutokea. Kila jambo linalotendeka katika jamii hutendeka mahali fulani na kazi za kifasihi nazo hufanya vivyo hivyo. Mandhari huweza kuwa halisi au ya kidhanifu. Mandhari na ujumbe hutegemeana kwa kuwa mtunzi asiposawiri mandhari vilivyo, ujumbe hauwezi kuwasilishwa kwa msomaji kikamilifu. Kwa mfano anapoeleza ujumbe kuhusu wanyonge, lazima atumie mandhari duni kama vile mitaa ya mabanda. Azma ya utafiti huu ni kuchunguza mchango wa mandhari ifaayo ili kufanikisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya mbili za Kiswahili *Rosa Mistika* (Kezilahabi) na *Maisha Kitendawili* (Habwe). Riwaya hizi zilichaguliwa kupitia usampuli wa kimakusudi na zimeandikwa na waandishi tofauti, mmoja wa nchi ya Tanzania na mwingine wa Kenya. Pia riwaya hizi ziliandikwa miaka ya 1971 na 2000 mtawalia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia inadai kuwa msanii anatarajiwa kutoa picha za matukio na mazingira halisi ambayo yanaonekana ili kuchora maisha kama yalivyo katika jamii. Kazi hii ilikuwa na malengo haya: kwanza, kubainisha mandhari mbalimbali yaliyochorwa na waandishi. Pili, kuchunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Mwisho, kutathmini ikiwa mandhari yaliyotumiwa na waandishi yameakisi hali halisi ya jamii. Utafiti huu umekuwa wa maktabani na data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia na matokeo yamewasilishwa kimaelezo. Utafiti uligundua kuwa mandhari ni muhimu sana kwa mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kikamilifu. Matumaini ya mtafiti ni kuwa utafiti huu utakuwa na manufaa kwa wahakiki, wasomi na walimu, wakuza mitaala na wanafunzi wa vyuo vikuu. Vilevile utachangia katika taaluma ya uhakiki na fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

**ABSTRACT**

The aim of every writer in Literature is to communicate to the readers or audience. In order to convey his message clearly, the writer uses different stylistic devices. Style refers to the ways a writer uses to convey his or her message. The message is communicated to the reader through the writer's style. Style involves the way the narration is done through the characters, literary devices used, setting and language. Setting is one of the aspects of style that shows place of the acts in the novel. Every event that takes place in the society happens at a specific place. The setting can be either real or imaginary. The setting and the theme depend on each other because if the writer does not use setting properly, he will not convey effectively to the audience, the message he intends to. For example, if the message is about less privileged in society, the writer must use the setting that portrays the status of the poor, like living in slums. The aim of this research was to investigate the role played by setting in building themes by using two Kiswahili novels, *Rosa Mistika* (Kezilahabi) and *Maisha Kitendawili* (Habwe). These two novels were selected using purposive sampling. The novels are written by two different authors, Kezilahabi and Habwe. They were written in different years, 1971 and 2000 respectively. This research was guided by Realism Theory. The theory argues that the writer should portray real life situations in the society. The objectives of the study are, first to analyze different settings portrayed and the messages in the two novels. Second, to investigate how setting was used in assisting the writers relay their messages. Finally, to evaluate the settings used by the writers in the two novels whether they portray real life situation. The data was collected through library research from the selected texts and other sources that expound the theory in use, then tabulated and analyzed. The findings were presented using descriptive presentation. The researcher hopes this research will be of great importance to researchers, readers, teachers, syllabus developers and students in universities. It will equally contribute to the field of Kiswahili literature.

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii tumefafanua usuli wa mada ya utafiti. Tumeeleza dhana ya mandhari na ujumbe kwa kuonesha uhusiano wake katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili.* Istilahi zote zilifafanuliwa na jinsi zinavyouhusiana na mada. Vilevile tumetoa madhumuni ya utafiti huu ili kubainisha malengo yetu. Pia tumeshughulikia maswali yaliyoongoza utafiti. Sababu za kuteua mada zimeelezwa kikamilifu. Nadharia iliyotumika imejadiliwa pamoja na mihimili yake.

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi ni nyenzo muhimu katika kuwasilisha ujumbe wa msanii kwa hadhira yake. Fasihi, iwe simulizi au andishi hukusudiwa aina fulani ya hadhira. Hadhira hiyo hupatikana katika mazingira maalumu katika jamii. Ili ujumbe uwe na mantiki na ukubalifu kwa hadhira lazima uakisi hali na matukio halisi ya hadhira lengwa.

Mwandishi anapoandika kazi yake huwa na ujumbe ambao hutaka uifikie jamii aliyoikusudia. Kazi ya fasihi huathiriwa na mazingira anamoishi mwandishi. Huchota yale yanayotokea katika maisha ya kila siku ya jamii yake. Kwa hivyo, mwandishi huandika juu ya yale yanayotokea katika hali halisi. Ujumbe huo unaweza kuwa na lengo la kuelimisha, kuonya, kutahadharisha kuburudisha au baadhi ya malengo haya. Ujumbe huo ni kipengele muhimu katika fasihi na hususan iwapo mwandishi anataka kazi yake iwe faafu katika jamii yake. Kazi yake hulenga kuifahamisha jamii yake yale yaliyomo ndani mwao, yawe mazuri au mabaya. Kwa hivyo ujumbe huo aghalabu unaweza kuakisi hali halisi ya jamii.

Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua kuwa mwandishi ni zao la jamii na hujaribu kuwasilisha matukio ya jamii katika uhalisia wake. Mwandishi huchota hadithi yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni kupitia fasihi tunapata picha kamili ya jamii.

Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kutumia vipengele vya fani. Vipengele hivi husaidia kuwasilisha ujumbe na pia kutia ladha hadithi yake. Haiwezekani kwa mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake bila ya kuitegemea fani. Fani hujumuisha wahusika, muundo, mtindo, lugha, mandhari, msuko na hata usimulizi.

Kazi ya fasihi inaweza kutumia wahusika, muundo, mtindo, lugha na mandhari ili kufikia lengo la mwandishi. Jambo hili hufanya kazi ya mwandishi kuwa tofauti na mwandishi mwingine. Vile vile utofauti wa tanzu za fasihi huwaelekeza wandishi kutumia fani zinazofaa ili kuwasilisha ujumbe wanaotaka. Ujumbe huu huwasilishwa kisanii. Usanii ni ufundi wa mwandishi katika kusuka hadithi yake.

Ufundi huu ni wa msanii wa kuumba kazi yake kutokana na ubunifu wake. Katika usanii huu mwandishi hutumia fani, na mandhari ni kipengele kimoja wapo. Kila aina ya mandhari husaidia kazi fulani ndiposa ujumbe uweze kuwasilishwa. Pia kipengele hiki hutumika pamoja na vipengele vingine kama vile wahusika. Umuhimu wa wahusika ni kuendeleza ujumbe mzima wa mwandishi hususan kutoa visa mbalimbali na mtiririko wa matukio mbalimbali kupitia mandhari mbalimbali. Wahusika hawa hukusudiwa kutenda matendo na matukio ambayo ni halisi katika mandhari halisi. Mandhari ni jinsi mahali panapoonekana na panapovutia macho au kukosa kuvutia (*Kamusi Elezi ya Kiswahili*,

2016:384). Mandhari ni sehemu mbalimbali ambazo mwandishi huonyesha matukio au sehemu alizopitisha wahusika wake.

Kulingana na Wamitila (2003:210) mandhari hueleza sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Anaongeza kwa kusema kuwa mandhari ina nafasi na umuhimu mkubwa katika riwaya na lazima msomaji ajitahidi kuangalia kama kuna uhusiano kati ya mandhari na vipengele vingine vya utunzi.

Mandhari ni mazingira ya wahusika pamwe na matukio. Inahusu mahali wanamokaa wahusika na kushirikiana. Mazingira haya ni ya kijamii, kiuchumi na nafsi za wahusika kitabaka (Njogu na Chimera, 2008:40). Hivyo kuelewa mandhari kulitusaidia kuelewa tabia za wahusika pamoja na ujumbe wa mwandishi.

Donna (1992) anaeleza mandhari kuwa ni uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi kwa kuwa humwezesha msanii kujenga hisia husika miongoni mwa wasomaji kwa kuyahusisha maelezo na mazingira husika. Mandhari inahusishwa na wahusika, ujumbe na mtindo uliotumika katika kazi yoyote ile ya kisanaa.

Katika utafiti huu, tulichukulia mandhari kuwa ni mahali maalumu mlimobuniwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi. Hivyo ili ujumbe kueleweka vizuri lazima mandhari yaakisi matukio yanayotokea kushadidia ujumbe. Utafiti huu ulichunguza mandhari yalivyotumika katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Maisha Kitendawili* (2000) kufanikisha ujumbe wa mwandishi.

### 1.2 Suala la Utafiti

Mandhari ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe katika kazi ya fasihi. Ujumbe au maudhui hufungamana na mandhari ili kukamilisha lengo la mwandishi. Kazi yoyote ya fasihi ina

ujumbe ambao mwandishi anataka kuupitisha kwa wanajamii. Ujumbe huu unatokana na mambo ambayo yanamkera mwandishi au anayaona yakitendeka katika jamii na anataka kuyapitisha kwa jamii fulani. Ujumbe huu hauwezi kufikia hadhira bila ya kipengele cha mandhari. Mandhari lazima yalandane na ujumbe wa mwandishi. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. Ulichunguza jinsi gani mwandishi amejenga au kuteua mandhari yake yalandane na ujumbe anaokusudia.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu yafuatayo:

i. Kubainisha aina za mandhari mbalimbali na namna yalivyochorwa na waandishi.

ii. Kuchunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi.

iii. Kutathmini iwapo mandhari yaliyotumiwa na waandishi yamesawiriwa kihalisia.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, waandishi wametumia mandhari ya aina gani kufanikisha ujumbe waliokusudia?

ii. Kipengele cha mandhari kina mchango gani katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi?

iii. Je, mandhari ya waandishi yamesawiriwa kihalisia?

### 1.5 Sababu za kuteua Mada

Ari ya kutaka kushughulikia utafiti huu ilitokana na sababu mbalimbali. Kwanza, jamii hubadilika kadiri ya wakati. Jinsi jamii inavyobadilika ndivyo mandhari yanavyobadilika. Vivyo hivyo usawiri wa mandhari katika kazi ya fasihi hubadilika. Katika jamii kuna mambo yanayochangia kubadilika kwa mandhari, mojawapo ni maendeleo ya teknolojia na kubadilika kwa njia za kujikimu kiuchumi. Mabadiliko haya huathiri mandhari pamoja

na ujumbe wa mwandishi kwa jamii husika. Kwa hivyo mada hii iliteuliwa ili kutathimini ikiwa mandhari hayo katika riwaya hizo mbili yameakisi hali halisi ya jamii ya msomaji.

Pili, kazi ambazo tulizishughulikia ni riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Maisha Kitendawili* (2000). Riwaya hizi ni za karne ya ishirini na ishirini na moja na ninatarajia zinaakisi hali halisi ya jamii ya msomaji kwa mujibu wa karne hizi. Kwa hivyo tumetathmini ikiwa mandhari zilizotumiwa na waandishi zinaakisi hali halisi ya jamii ya msomaji au la katika karne hizi mbili.

Sababu nyingine ni kuwa katika fasihi andishi kipengele cha mandhari ni cha kimsingi katika riwaya. Katika utanzu wa tamthilia na ushairi mandhari hutumika kwa njia tofauti. Upana wa matumizi ya mandhari katika riwaya ndiyo sifa iliyotupatia ari ya kuchuguza aina mbalimbali za mandhari zilizotumika katika riwaya teule. Pia utafiti ulibainisha iwapo mandhari na ujumbe wa waandishi hawa unalandana kikamilifu.

Sababu nyingine ni kuwa mtafiti amechunguza ikiwa waandishi Euphrase Kezilahabi na John Habwe kama waandishi wa fasihi, wametumia vipi kipengele cha mandhari katika kufanikisha ujumbe wao. Wametumia njia za kipekee au la? Sifa hii ndiyo iliyotupa ari ya kuchunguza mchango wa mandhari hayo katika kuwasilisha ujumbe katika riwaya za*Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*.

Mwisho, mtafiti alichagua mada hii kwa kutambua kuwa hakuna utafiti uliofanywa kuhusu mchango wa mandhari katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. Kwa sababu hii ikawa muhimu katika kubainisha mandhari mbalimbali zilizotumika na waandishi kufanikisha ujumbe katika riwaya teule.

### 1.6 Upeo na mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ni wa kifasihi na unahusu utanzu wa fasihi andishi. Tanzu za fasihi andishi ni pamoja na riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Uchunguzi huu ulihusu utanzu wa riwaya. Riwaya zilizochunguzwa ni mbili, zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi na John Habwe. Riwaya zenyewe ni ni *Rosa Mistika* (1971) na *Maisha Kitendawili (2000)*. Katika kazi hii tulilenga kubainisha mandhari mbalimbali yaliyochorwa na ujumbe wa waandishi katika riwaya hizi teule. Pia tulitathmini iwapo mandhari yaliyotumiwa na waandishi yameakisi hali halisi ya maisha ya jamii. Utafiti huu ulichunguza tu mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Vipengele vingine vya fani havikushughulikiwa.

### 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Kulingana na Msokile (1993) maana ya nadharia ni dhana au mpango uliowekwa ili kusuluhisha jambo fulani. Mpango huu ulituongoza katika utafiti huu kwa ajili ya kufanikisha malengo. Wamitila (2002), anaeleza nadharia ni wazo kuu au mwongozo uliowekwa kwa ajili ya utenda kazi fulani.

Nadharia ni mambo yote ambayo humsaidia mhakiki na msomaji kuielewa fasihi kwa kuzingatia kanuni fulani. Nadharia humwongoza mhakiki au mwandishi wa kazi ya fasihi kuelewa ujumbe vizuri, kutambua vipengele vya fani na kutumia vipengele hivyo kwa njia mwafaka yenye uwiano katika kazi ya fasihi. Kama vile mandhari yanavyolingana na wahusika katika kazi ya fasihi (Njogu na Wafula, 2007).

Massamba (2009:63) anasema, “Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo

cha kuelezea jambo." Kwa hivyo, nadharia ni wazo kuu au miongozo iliyowekwa kwa ajili ya wahakiki na waandishi wanaposhughulikia kazi ya fasihi.

Katika sanaa uhalisia huashiria uhusiano kati ya uumbaji wa msanii na ulimwengu halisi. Kitu chochote kinachoumbwa na msanii kwa kiwango fulani kinajikita katika sura ya chombo hicho kama kionekavyo katika uasili wake. Kwa mfano, msanii wa Kigiriki aitwaye Zeuxis alionyesha ufundi mkubwa alipochonga sanamu ya mvulana anayebeba zabibu, alionekana na uhalisi zaidi hata ndege walikuja kudona zabibu hizi wakifikiri ni zabibu halisi.

Uhalisia huthamini ulimwengu wa vifaa, matukio na visababishi vinavyoonekana vya matukio hayo na kuwajibika kuyaeleza kwa usahihi, kikamilifu na zaidi ya hayo na akili timamu bila upendeleo. Katika maisha ya kila siku, mtu ambaye anaangalia ukweli kwa akili timamu bila upendeleo na ubinafsi kama iwezekanavyo na anakataa kuyumbishwa katika uamuzi wake kwa matumaini au hofu, mara nyingi huitwa mhalisia (*Colliers Encyclopedia, Volume* 16).

### 1.7.1 Nadharia ya Uhalisia

Uhalisia ni mkondo unaosisitiza usanii wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Katika sanaa uhalisia huashiria uhusiano kati ya uumbaji wa msanii na ulimwengu halisi. Kitu chochote kinachoumbwa na msanii kwa kiwango fulani kinajikita katika sura ya chombo hicho kama kionekavyo katika uasili wake.

Nadharia hii ilianza huko Ufaransa ambako wandishi kama vileGustave Flaubert (1850), walitumia dhana ya uhalisia kuelezea kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu

jinsi yalivyo na uigaji wa mazingira wanamopatikana wanadamu (*Encyclopedia Britannica Volume* 9).

Katika karne ya 19, katika historia, istilahi uhalisia huelekezwa kwa sanaa za mchoraji Mfaransa aliyejulikana Gustave Flaubert ambaye michoro yake iliwatia kiwewe Wafaransa (Qusby, 1998). Alidai kuwa uhalisia ni kuondoa ufaraguzi mwingi na kuangalia dunia kwa uamilifu na usawa kutokana na tajriba na uzoefu wa kibinafsi. Flaubert aliungwa mkono na wafuasi wa Fernard. Chanzo cha nadharia hii kilikuwa matokeo ya misukosuko ya mapinduzi yaliyotokea mwaka wa 1878 huko ufaransa, hasa yale mapinduzi ya kisiasa na kiuchumi. Nadharia hii ilizuka kama njia ya kupinga ulimbwende. Ulimbwende ulihusu mambo yasiyowezekana na ya kinjozi. Hata hivyo uhalisia katika kazi za sanaa ulipendekezwa na Plato takriban miaka mia nne (400) kabla ya Masihi. Plato alisema kwamba msanii aandike au kuchora yale mambo halisi yanayopatikana katika jamii (Gilbert Allan, 1962).

Walimbwende walikuwa wakijitungia mambo wasiyoweza kutimiza. Jambo hili lilifanya wao kuchukuliwa kuwa waliishi ndotoni. Kutokana na hili wahakiki na watunzi walianza kuwadhihaki walimbwende (Njogu na Wafula, 2007: 61).

Kulingana na Msokile (1993: 106) uhalisia ulianza mwaka wa 1820. Msokile anasisitiza kuwa kazi yoyote ya fasihi inatarajiwa kuonyesha mazingira halisi na itaje mambo yanayodhihirika katika jamii. Isitoshe, kazi hiyo itumie wahusika wanaoonyesha hali halisi ya jamii. Mhusika awe wa kawaida na kupatikana katika mandhari ya kawaida. Kwa hivyo, dhana ya uhalisia hutumiwa kuelezea aina ya mtazamo wa kifasihi unaochukulia kazi za kifasihi kama zinazoakisi sifa ya kimsingi inayohusishwa na uhalisia.

Naye Mbatia (2001:92) anasema kuwa uhalisia ni tapo la uandishi lililozuka Ulaya katika karne ya kumi na nane (18) na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu. Anaendelea kusema kuwa wasanii wa kiuhalisia walijishughulisha kuutafuta na kubainisha ukweli wa maisha. Waliamini kuwa ukweli huo uliweza kupatikana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Hivyo basi walijikita katika mazingira halisi ya kijamii na kujaribu kuyasawiri kama yalivyo bila kupotosha.

Uhalisia ni dhana ya kiyakinifu na pana ambayo husisitiza pakubwa kuhusu hali za kawaida za maisha ya binadamu, mandhari anakoishi na maisha yake. Mawazo yake hayatengenezwi kwenye dhana ya dhahania kama urembo, hadithi za majitu au ndoto bali yanatengezwa katika hali halisi inayoonekana. Kama nadharia ya uhakiki, uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali, jinsi ya kuusawiri na kuuelewa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine (Wamitila, 2006). Kutokana na jambo hilo tunaweza kusema kila kikundi katika jamii kina uhalisia wake.

Wafula (2012), alieleza kwamba waandishi ambao hutumia uhalisia katika sanaa zao hujikita katika kuonyesha ukweli bila kutumia fantasia. Kazi ya mwandishi huthaminiwa kulingana na vile alivyoonyesha uwazi wa mambo katika jamii. Kwa hivyo, uhalisia ni kusawiri mambo kama yaonekanavyo katika ulimwengu bila kutia chumvi. Uhalisia huu katika riwaya huonyesha uhusiano wa yale yanayotokea katika riwaya na yale yanayotokea katika maisha ya kila siku, kwa kuwa ni mambo yanayoweza kukubalika na kuelezeka.

Wasanii wanaotumia uhalisia hujikita katika kutumia wahusika ambao wanaonekana katika hali halisi ya jamii. Pia, wahusika huendelezwa vile ambavyo hupatikana katika mandhari ya kawaida wakati wasanii wanapoandika hadithi zao (Njogu na Wafula, 2007).

Kulingana na maelezo haya, fasihi hasa riwaya na tamthilia hutarajiwa sanana wasomi ziwe na wingi wa ukweli na uhalisia. Jambo hili linaonekana kuwavutia na kuwapendeza wengi ambao wanataka kujua ukweli unaotendeka katika jamii husika. Fauka ya hayo fasihi ni kioo cha jamii kwamba imulike yaliyoko kwenye jamii ili kuzindua na kukosoa. Waasisi wa nadharia ya uhalisia walitambua kuwa kuna uhusiano katika ya kazi ya mwandishi na mandhari yake. Jambo hili lilisababisha waasisi hao kutaka kudhibitisha uhusiano huo (Lukacs,1972). Nadharia hii ya uhalisia hutumika katika kuchanganua kazi ya mwandishi kwa lengo la kubaini uhalisia wake na umuhimu wake.

### 1.7.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia

i. Kazi ya mwandishi inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Uhalisia sharti ujihusishe na mambo halisi yanayotokea katika mazingira halisi.

ii. Msanii anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake. Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi fulani cha historia na kuyatumia kuwasilisha ujumbe wake.

iii. Mandhari katika kazi za fasihi, zidhihirishe ukweli wa maisha halisi. Mwandishi atumie mandhari halisi.

iv. Uhalisia unapinga maandishi ya kilimbwende.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeeleza yale yaliyoandikwa na yanayohusiana na utafiti huu. Tulipitia vitabu, magazeti na tasnifu mbalimbali ambazo zimezungumzia yaliyolingana na mada yetu. Tulipitia yaliyoandikwa kuhusu ujumbe na mandhari. Vile vile tulipitia tafiti mbalimbali zilizofanywa juu ya fasihi, hususan zilizokaribiana na mada yetu na kuonyesha mchango uliotoka kwa tafiti hizo. Pia tulibainisha tofauti zilizopo kati ya tafiti hizo na utafiti wetu. Kazi hii iligawanywa katika sehemu mbili: maandishi kwenye vitabu na tasnifu.

## 2.1 Vitabu

Jameson (1981) alishughulikia kazi ya fasihi katika jamii. Yeye alidokeza kuwa tofauti ambazo huwa kwenye jamii hutokana na mivutano ya mambo ya kiuchumi na ulafi baina ya tabaka la juu (matajiri) na tabaka la chini (maskini). Tofauti hizi zinaweza kusababisha vita ambavyo hutokea juu ya raslimali za nchi, mishahara duni, kazi zizizokuwa za kudumu, mazingira duni ya kazi na pia kupigwa kalamu wakati wowote. Utafiti huu ulitufaa kwa sababu ulituelekeza kufahamu na kupambanua ujumbe wa Euphrase Kezilahabi na John Habwe katika riwaya zao kupitia migogoro katika riwaya hizo.

Katika kuhakiki fasihi, ili fasihi kueleweka na kuwa na mnato, lazima iwe na msingi unaoimiliki. Sababu kazi ya wanafasihi hawa inamulika uhalisia fulani, kwa hivyo mandhari hayana budi kuwa kwenye kazi hiyo. Kazi ya fasihi hutegemea jinsi ilivyoandikwa au kutungwa. Kipengele cha mandhari huwa muhimu katika kuelewa kazi

ya mwandishi. Matumizi mazuri ya mandhari katika kazi ya mwandishi husaidia msomaji kuifahamu na kuielewa kazi husika barabara. Mandhari ni sura ya mahali na jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Mwandishi hutumia mandhari kuonyesha mazingira halisi na uhalisia wa kile anachozungumzia kwenye fasihi yake. Isitoshe, mwandishi wa fasihi hutumia picha halisi za mabanda kutuonyesha jinsi eneo hilo lilivyokuwa na nyumba za karatasi na uchafu uliopo.

Ujumbe wa mwandishi unaweza kutokeza iwapo vipengele vya mandhari na wahusika vimeambatana vilivyo. Mfano, iwapo mtunzi atasawiri mhusika maskini hohehahe, atatuonyesha sehemu duni anayoishi, mateso anayopitia na ugumu wa maisha kama dhihirisho halisi ya umaskini (Mwenda Ntarangwi, 2004). Kwa hivyo mandhari ni kigezo muhimu kwa kuhakiki riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. Kazi yoyote ya mhakiki lazima iongozwe na maswali haya: Je, mwandishi amechora wahusika na mandhari yanayowasilisha ujumbe wake? Pia mandhari haya yanaonyesha hali halisi ya jamii katika maisha ya sasa?

Kulingana na Mwenda (2004) anasema kuwa wahakiki hushughulikia mambo mawili makuu katika fasihi, yaani ujumbe na fani. Ujumbe ni yale yanayotiliwa mkazo katika riwaya nzima kutoka mwanzo hadi tamati. Riwaya inaweza kuwa na maudhui mbalimbali. Kinachozungumziwa katika kazi ya fasihi ndio ujumbe. Kazi ya fasihi inaweza kuwa na ujumbe mbalimbali kama Dhuluma katika jamii, Elimu, Tamaa, Dini, mikinzano katika Ndoa, Umaskini unavyojitokeza na kuathiri jamii na Mabadiliko ya tamaduni. Ujumbe huu hutoa picha halisi ya binadamu katika jamii inayozungumziwa na mwandishi. Pia, kuelewa wakati mwandishi alipoandika kazi yake ni muhimu sana katika kuhakiki kazi za fasihi. Wakati huu utamsaidia msomaji kuelewa uhalisia wa ujumbe, pia kuueleza ujumbe wake.

Kubadilika kwa utamaduni wa binadamu kupitia muda mrefu na mwendo wa jamii kiwakati ni swala ambalo mwandishi anapaswa kutia maanani kwa kuwa yaliyopita hufungamana na mambo mengi yajayo na yatokeayo. Yaliyopita huenda yakamkumba binadamu katika maisha yajayo. Kwa hivyo, katika kuelewa wakati alipoandikia kazi, mwandishi huweza kufahamu ujumbe na kuuendeleza vizuri. Maelezo haya yalituwezesha kutambua kipindi cha historia walimotungia kazi zao Euphrase Kezilahabi na John Habwe na kutambua mandhari ya wakati yaliyodhihirika katika kazi zao.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa umuhimu wa fasihi ni kuwaelimisha wanajamii na kuwawezesha kutambua yale yanayoendelea. Pia fasihi itazindua na kumwamsha msomaji fikra na hisia zake. Fasihi inayomulika shida wanazopitia wanajamii huwapa maarifa wanajamii hao na kuweza kuzibadilisha hali zao za maisha. Hali hii inadhihirika katika riwaya mbili teule.

Maudhui au ujumbe una njia mbili ambazo zinauhusiana. Kwanza maudhui ni mambo yanayozingatiwa kwenye fasihi yoyote. Mambo haya hutegemea vile ambavyo mtunzi ataiendeleza kazi yake. Pia maudhui ni kukirejelea kiwango cha maana ya kazi ya fasihi (Wamitila, 2008). Kwa mjibu wa Gatakaa (2012) ujumbe ni yale yanayojitokeza katika kazi nzima ya fasihi.

Kwa hivyo kwa kuegemea fafanuzi zetu tunakubaliana na wataalamu hao na kusema kuwa ujumbe ni mawazo muhimu yanaojitokeza katika kazi ya fasihi. Kila kazi ya fasihi huzungumzia jambo fulani. Katika fasihi mwandishi anastahili kueleza maisha halisi ya wahusika wanaozungumziwa kwa kuwa mwandishi anaandika kuhusu jamii husika naye ni mwanajamii ndani ya jamii hiyo. Ataandika kuhusu jamii husika kwa kuegemea maisha

ya jamii hiyo kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kuzingatia wakati maalum wa kihistoria. Kwa hivyo, ujumbe wa wandishi Euphrase Kezilahabi na John Habwe ndio tuliouchunguza katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*.

## 2.2 Tasnifu

Kamunde (1983) alitumia riwaya za *Utengano* (1980), *Asali Chungu* (1978) na *Dunia Mti Mkavu* (1980) kuelezea tofauti za kiuchumi zilizopo baina ya matabaka mawili (la juu na la chini). Kamunde alijadili aina za wahusika na jinsi wanavyoonyesha udhaifu katika kazi zao. Kupitia riwaya za Said Ahmed Mohammed, Kamunde anazungumzia mambo yanayowakandamiza wanyonge. Maswala anayotaja ni uchumi, siasa na mambo ya kijamii. Utafiti huu wa Kamunde ulikuwa muhimu kwetu kwa sababu aliangazia mambo yanayoshuhudiwa katika jamii ya sasa.

Lugano (1989) amehakiki kazi ya Kezilahabi na kuonyesha jinsi alivyowaumba wahusika wa kike kwa kuzingatia mambo matatu, uchumi, siasa na jamii. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa mwanamke alionekana kama kiumbe duni, kifaa tu cha kuuzima uchu wa mwanamume. Kazi yake ilitufaa kuelewa jinsi mwanamke alivyochorwa na wandishi wengine na umuhimu wao katika kazi hizo walizoandika.

Kazi nyingine iliyokuwa na umuhimu kwa utafiti huu ni ya Muindi, J. (1990) aliyechunguza “Usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya za Said Ahmed Mohamed”. Alichunguza jinsi wanawake walivyosawiriwa kama makahaba na kutoa sababu zake. Utafiti huu ulitufaa kwa sababu ulionyesha namna mandhari yanavyoweza kuchochea mielekeo mibaya kama ukahaba.

Moser (1993) katika Gender Planning and Development amechunguza mgao wa kazi za nyumbani. Moser amesema kwamba majukumu ya uzazi hujumuisha kuzaa, kulea watoto na shughuli nyingine ambazo ni muhimu katika familia. Majukumu haya huhusishwa na wanawake, na kazi hizi zinahitaji muda mrefu na uvumilivu sababu mara nyingi ni za kurudiarudia. Maswala aliyoyatafitia yatatusaidia kuelewa mambo tunayoyachunguza ingawaje tunamulika kazi tofauti.

Naye Khaemba (1999) alitafitia kuhusu “Ulinganishi wa maudhui ya mapinduzi katika Dunia Mti Mkavu na Kiza katika Nuru”. Khaemba anaeleza kwamba uhalisia wa kijamaa hueleza maisha kuwa vitendo vya uzalishaji ambavyo huleta manufaa katika jamii bila kikwazo fulani. Maswala ambayo Khaemba aliyoyatafitia yatatusaidia kuelewa mambo tunayoyachunguza ingawaje tunamulika kazi tofauti.

Nao utafiti wa Nkonge (2006) umeshughulikia athari za udhanaishi katika riwaya za *Kichwa Maji* na *Nguvu ya Sala*. Nkonge alishughulikia mambo kama ndoa, mapenzi, uozo wa jamii na dini akilenga vijana. Masuala haya yanaoana na baadhi ya yale tulishughulikia katika utafiti wetu. Maswala aliyoshughulikia yataufaa utafiti wetu. Nkonge alitumia nadharia ya udhanaishi katika utafiti wake na sisi tulitumia nadharia ya uhalisia.

Katola (2006) alichunguza, “Udhalimu Dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili”. Masuala muhimu aliyoyashughulikia yalikuwa ujumbe wa kinjisia jinsi unavyojitokeza kupitia sura yake na taswira ya mwanamke na matumizi yake katika uandishi wa fasihi. Kazi ya Katola ilihusu dhuluma kwa jinsia ya kike. Utafiti huu ni tofauti na wetu ila ulitusaidia kuhakiki ujumbe wa udhalimu katika kazi ya Euphrase Kezilahabi na John Habwe.

Katika tasnifu ya Kweyu (2007) kuhusu “A Critical Analysis of Patriarchy and Masculinity in Kezilahabis *Rosa Mistika* and *Kichwamaji*”, Alitathmini kuhusu ubabedume. Alisema mojawapo ya mambo yanayochangia katika kudhulumiwa kwa mwanamke ni utamaduni. Pia amedhihirisha jukumu la vijana katika jamii zinazodhulumu wanawake. Utafiti huu ulitusaidia katika kufafanua ujumbe wa Euphrase Kezilahabi na John Habwe kwa kuonyesha jinsia ya kiume inavyojitambulisha kupitia kipengele cha nguvu za kiume katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*.Maswala aliyoyatafitia yatatusaidia kuelewa mambo tunayoyachunguza ingawaje tunamulika kazi tofauti.

Nyaosi (2008) amechunguza taswira ya Asasi ya Ndoa katika riwaya ya *Kiu* na *Msimu waVipepeo*. Katika utafiti huu, Nyoasi ameshughulikia dhuluma na ukandamizaji wa mwanamke katika asasi ya ndoa. Ameonyesha matatizo yanayowakumba wanawake katika asasi ya ndoa. Utafiti huu ulitusaidia kuelewa dhuluma wanazopitia wanawake katika ndoa na dhuluma hizi hutokea katika mandhari yepi. Utafiti huu wa Nyoasi alishughulikia kipengele cha taswira nasi vipengele vya mandhari na ujumbe.

Tambasi (2011) katika kazi yake alitumia nadharia ya umuundo katika kuchunguza fani kwenye utenzi. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa kuwa ilituongoza kuelewa zaidi kuhusu vipengele vya fani. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa sababu yeye aliangazia utenzi wa Tambuka ilhali sisi tulihakiki riwaya za *RosaMistika* na *Maisha Kitendawili.*

Muusya (2012) amechunguza mandhari katika hadithi fupi katika diwani za *Pendo la Heba* na *hadithi nyingine na Mizungu ya Manabii na hadithi nyingine*. Katika utafiti wake Muusya amechunguza jinsi waandishi wanavyosawiri mandhari katika hadithi fupi na jinsi

wametumia lugha katika hadithi hizo. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa ulitupa mwanga kuhusu kipengele cha mandhari.

Obure (2012) amechunguza, "Dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini".* Kupitia utafiti wake amedhihirisha kuwa jinsia ya kike inapitia madhila mengi katika jamii. Ni kupitia kazi hii tulitambua mandhari ambayo jinsia ya kike inadhulimiwa. Picha hii ya mandhari ilituelekeza kutambua mandhari mbalimbali katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili.*

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imefafanua mbinu ambazo mtafiti ametumia katika kazi yake. Mbinu hizi ni pamoja na njia zilizotumika kukusanya data, usampuli, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Kothari, (2004), anaeleza kuwa mbinu za utafiti huwa jumla ya mbinu zote ambazo mtafiti hutumia wakati wa utafiti. Mbinu hizi zinajumuisha uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data na uwasilishaji wa data.

## 3.1 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Ili kuafikia madhumuni yetu tulisoma riwaya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* mara kadhaa. Pia tulisoma vitabu vya nadharia ya uhalisia. Vile vile, vitabu vinavyozungumzia mbinu za kisanii kwa ujumla na hasa kipengele cha mandhari. Tafiti za awali zenye mada zinazohusiana na utafiti huu zilipitiwa. Tulifanya upekuzikwenye mitandao kuona ni makala yapi yalitufaa kulingana na malengo yetu. Tuliyasoma na kuyajumlisha katika kazi yetu. Mtafiti pia aliogozwa na malengo ya utafiti.

## 3.2 Usampuli

Sampuli ya utafiti huu ni ya kimakusudi. Sampuli ya kimakusudi humpa fursa anayefanya utafiti kuchagua eneo na mahali pa utafiti (Mugenda, 1999). Kwa hivyo, tuliteua riwaya za Eupharse Kezilahabi na John Habwe. Waandishi hawa wametoka katika mataifa mawili tofauti ambamo Kiswahili kimeendelezwa sana. Euphrase Kezilahabi ni mtanzania na John Habwe ni mkenya. Waandishi hawa wameandika riwaya mbalimbali kwa mfano Euphrase Kezilahabi aliandika *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo*

(1975), *Gamba la Nyoka* (1979), *Nagona* (1990). John Habwe aliandika *Maumbile si Huja* (1995), *Maisha Kitendawili* (2000), *Paradiso* (2005), *Cheche za Moto* (2008), *Fumbo la Maisha* (2009), Pamba (2011), *Safari ya Lam*u (2011), *Kovu Moyoni* (2014) na *Hidaya Yangu* (2018). Lakini mtafiti aliteua kimakusudi riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* kwa kuzingatia kuwa vitabu hivi vinaangazia matatizo ya wanawake katika jamii, vimetengana kiwakati kwa miongo kadhaa na zote mbili zinasawiri mazingira anuwai. Sampuli hii ilitosheleza data iliyohitajika katika utafiti huu.

### 3.3 Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na vifaa kama kalamu, daftari na tarakilishi vilitumika. Vifaa hivi vilitumika na vilikuwa na umuhimu sana katika utafiti huu. Daftari pamoja na kalamu zilitumika kunakili habari mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti. Chochote tulichosoma katika maktaba ambacho kilihusiana na mada yetu ya utafiti kilinakiliwa kupitia kalamu na daftari.

Tarakilishi ilitumika kwa kiwango kikubwa katika utafiti huu. Tarakilishi ilisaidia kutafitia kupitia mtandao na kuhifadhi data mbalimbali. Machapisho, tasnifu na taarifa muhimu zinazohusiana na mada kwenye mtandao zilitafitiwa kupitia tarakilishi.

### 3.4 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kimaelezo. Data hiyo ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Hatua zifuatazo zilizingatiwa katika kuchanganua data. Kwanza mtafiti alisoma riwaya za*Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*na kuchambua mandhari mbalimbali yaliyotumika katika riwaya zote mbili. Hatua ya pili ni mtafiti alichunguza mchango wa

mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Mandhari yaliyotumika na waandishi Euphrase Kezilahabi na John Habwe yameelezwa jinsi yanadhihirisha ukweli wa maisha halisi ya binadamu.

### 3.5 Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kupitia njia ya maelezo, kwa kuzingatia malengo ya utafiti na nadharia ya uhalisia. Maelezo haya yalizingatia ufafanuzi wa aina za mandhari yaliyotumika katika riwaya teule, kudondoa mchango wa mandhari hayo katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya uhalisia, utafiti umebainisha uhalisia wa mandhari na ujumbe kwa kudhihirisha hali halisi ya maisha ya jamii hizo.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia kubainisha mandhari mbalimbali yaliyochorwa katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*. Pia tumeshughulikia ujumbe unaotokana na mandhari hayo katika riwaya zote mbili. Sehemu hii tumebainisha jinsi mandhari yanavyochangia katika kufaulu kwa ujumbe wa mwandishi. Kisha tumetathmini iwapo mandhari yaliyotumiwa na waandishi yameakisi hali halisi ya jamii.

Mandhari ni muhimu katika kazi ya fasihi kwa sababu zifuatazo. Mandhari huwezesha ujenzi wa migogoro katika kazi yoyote ya fasihi. Migogoro hii hutokea baina ya wahusika waliopo katika mandhari yale au waliopo katika mandhari tofauti. Migogoro hii ndiyo inayozua ujumbe wa mwandishi. Pia mandhari hutuwezesha kuhisi au kupata tajiriba ya yale mwandishi anayotaka kupitisha katika jamii. Mwandishi anapotumia mandhari fulani huwa ametutoa ulimwengu wa kiubunifu hadi ulimwengu wa kiuhalisia. Msomaji wa fasihi huweza kuchora picha halisi zinazohusiana na kazi ya mwandishi. Katika utafiti huu, tumechukulia mandhari kuwa ni mahali maalum mlimobuniwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi. Mandhari hayo hujumuisha wakati na mazingira ambamo wanajamii hutangamana. Utafiti huu umechunguza mchango wa mandhari kama kipengele cha fani katika kufanikisha ujumbe wa wandishi katika riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*.

### 4.1 MANDHARI YALIVYOSAWIRIWA KATIKA *MAISHA KITENDAWILI*

Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* mwandishi amesawiri mandhari ya aina mbalimbali ili kufanikisha ujumbe wake. Mandhari haya nimeyainisha katika aina tatu. Mandhari ya

mahali, mandhari ya wakati na mandhari ya hali. Aina hizi ndizo ambazo zimechanganuliwa na kuonyeshwa zinavyojitokeza katika riwaya teule.

### 4.1.1 Mandhari ya mahali

Mandhari ya mahali huelezea ni wapi tukio hutokea. Kila kisa katika fasihi huwa na sehemu tofauti na huwa na mandhari tofauti. Mahali pa pekee panaweza kutumiwa kutoa asili ya mgogoro mpya. Pia mandhari ya mahali yanaweza yakachukua dunia, nchi, jiji, mji, kijiji, kitongoji na ndani ya nyumba. Mandhari ya mahali katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* yanajitokeza pale ambapo mwandishi anaelekeza wahusika wake ili kufanikisha ujumbe wake. Mandhari haya yanadhihirika kwa njia mbalimbali.

#### 4.1.1.1 Mandhari ya Nyumbani

Mwandishi ametuchorea mandhari ya nyumbani katika sehemu zifuatazo. Kwanza nyumbani kwa mhusika Papi. Kupitia mhusika Papi tunapata picha halisi ya nyumba yake jinsi ilivyojengwa na kupambwa. Ilikuwa nyumba ya kifahari ambayo ilikuwa na ukumbi mkubwa wa kuvutia. Katika ukumbi huo, chini sakafuni kulirembeshwa kwa zulia jekundu. Pia kulikuwa na viti vya bei ghali. Kwenye paa la nyumba hii, taa ya stima ilining'inia kama tunda la mkoma. Ukutani picha ya Papi ilikuwa kwenye upande wa matlai, na upande mwingine wa ukuta kulikuwa kumesimama kabati jeusi refu lililotiwa mapambo likawa linavutia. Mwandishi anaeleza taswira aliyoiona Farida alipoingia nyumbani kwa Papi:

> "…Farida alijikuta katika ukumbi mkubwa wa kuvutia katika jengo
> moja. Chini kulirembwa kwa zulia jekundu. Viti vya heba vimekaa
> na kutulia. Taa ya stima iliyokuwa ukumbini humo ilining'inia kama
> tunda la mkoma…" (uk. 21).

Mandhari haya ya nyumbani kwa mhusika Papi yanatufichulia ujumbe wa utabaka. Familia hii ni ya tabaka la wenye mali kwani waliishi katika jumba la kifahari mno. Pia vitu

vilivyopatikana kwenye nyumba ya mhusika Papi ni dhahiri kuwa alikuwa na pesa za kununua vitu vya bei ghali.

Mandhari ya nyumbani pia yamejitokeza kupitia wahusika Kasu na Yasmini. Kasu na Yasmini waliishi kwenye maskani duni. Chumba walichoishi mlangoni mlikuwa na pazia la chandarua iliyochanwa, ilikusanya rangi nyingi hadi kutambua rangi halisi ilikuwa ngumu. Kazi walizofanya zilikuwa na mapato duni. Kasu alikuwa muuza makaa kwenye kibanda. Pesa walizopata kutokana na biashara hii ya kuuza makaa hazikutosha kulipia nyumba kodi. Jambo hili lilisababisha Kasu na Yasmini kufanya kazi ya" nipe-nikupe" yaani ukahaba ili wapate pesa za kulipa kodi ya nyumba:

> "…Kasu na Yasmini hufanya nipe nikupe mpaka wakadunduliza
> ngwenje kulipa kodi. Wakati fulani hulipa shilingi tano na
> wakamshtakia tajiri na kumwambia wanatarajia nyingine kutoka
> kwa wateja…" (uk.26).

Kazi walizofanya hazikuwa na mapato ambayo yangewawezesha kununua pazia nzuri. Mandhari haya ya nyumbani kwa Kasu na Yasmini yametumika na mwandishi kuwasilisha ujumbe wa utabaka ambao unasababisha wahusika kutafuta njia mbadala za kujikimu kimaisha.

Mandhari ya nyumbani kwa Bwana Omar yametumiwa kuwasilisha ujumbe wa utabaka. Familia hii ilikuwa ya tabaka la maskini. Jambo hili linadhihirika kupitia mambo yafuatayo. Kwanza, familia ya Omar haikuwa na pesa za kumpeleka Bwana Omar hospitali kupata matibabu. Hili lilimfanya kila mmoja katika familia hii kuzoea hali ya taabu ya Bwana Omari na hasa wakati wa mvua na kipupwe (uk.32). Wakati mzee Omar anazidiwa na ugonjwa usiku, mkewe Kibibi anatumia maji baridi ya kumzindua aliyoyatia kwenye

karai iliyokuwa inavuja. Zaidi ya hayo, mwandishi anaonyesha jinsi chumba cha watoto wa Bwana Omar kilivyokuwa. Pili familia ya Bwana Omar haikuwa na uwezo wa kujenga nyumba yenye vyumba vya kutosha vya kulala. Wanawe Farida na Kasu walilala katika chumba cha kupumzika. Matandiko waliyoyalalia yalikuwa makuukuu na yaliongezewa magunia yaliyozeeka. Pia matandiko hayo yalikuwa yameliwa na mchwa. Kutokana na mambo haya ni dhahiri kuwa familia hii ya Bwana Omar ilikuwa maskini:

> "…Huko katika chumba cha kukaa ndiko Farida walikokuwa wamelazwa
> kwa jamvi kuukuu iliyotandikwa magunia na maleso yaliyozeeka.
> Jamvi hili lilichekesha lilivyokuwa limeliwa na mchwa…" (uk.34.)

Mandhari ya nyumbani pia yanajitokeza kwa mhusika Mama Josii. Kupitia mhusika Kasu tunapata picha halisi ya nyumbani kwa Mama Josii. Familia ya mama Josii ilipitia hali ngumu ya maisha. Watoto wa Mama Josii walilala sakafuni ambapo palitiwa jivu. Zaidi ya hayo, watoto hao walitandikiwa karatasi ambazo walizitumia kama gondoro (uk.67). Taa iliyotumiwa katika familia hiyo ilikuwa ya kibatari. Nyumba pia ilikuwa inavuja maji paani na ukutani. Jambo hili linaashiria kuwa msimu wa mvua familia hii ilitaabika kwa kuwa maji yalilowa kila mahali kwenye nyumba hiyo. Kupatikana kwa chakula katika nyumba ya mama Josii ilikuwa taabu. Mama Josii ndiye aliyekuwa tegemeo la pekee katika familia hiyo, kwani mumewe alikuwa mgonjwa na hakuwa na uwezo wa kufanya kazi. Jukumu la kutunza familia liliachiwa mama Josii pekee. Kwa hivyo, Mama Josii alijikakamua kulea watoto ambao mwandishi anatudokezea walikuwa shule nzima yaani walikuwa wengi. Familia hii haikuwa na pesa za kumpeleka mumewe Mama Josii hospitali kupata matibabu. Mumewe Mama Josii aliugua kwa miaka saba bila kupata matibabu yoyote kwa kuwa familia hii haikuwa na uwezo wa kumpeleka kulazwa hospitali. Watoto wake Mama Josii,

Agnes na Jane hawakuwa wanaenda shule licha ya wao kutimiza umri wa kuenda shule (uk.69). Kutojiunga na shule kulitokana na Mama Josii kukosa karo ya kuwapeleka shuleni. Mambo haya yanadhihirisha kuwa familia ya Mama Josii ilipitia hali ngumu ya maisha na hivyo ilikuwa miongoni mwa tabaka la maskini.

Mandhari ya nyumbani pia yamedhihirika nyumbani kwa Bwana White. Mwandishi anatuonyesha picha halisi ya nyumba ya Bwana White, kuashiria kuwa Bwana White alikuwa mwenye mali na aliishi maisha ya kifahari. Mwandishi anatudokezea kuwa jumba hilo alikoishi Bwana White lilijaa uzuri wa kila aina. Jumba lake lilizungukwa na waya wa kichungi, mbele kulikuwa na miti ya aina ya mivinde. Paa la nyumba lake lilikuwa la kifahari na madirisha yalikuwa makubwa na yalitiwa vitambaa vya bei. Isitoshe, vyuma vya madirisha hayo viliagizwa kutoka ng'ambo (uk.83). Bwana White pia alikuwa na wafanyakazi mbalimbali. Alikuwa amemwajiri mlinzi na pia alikuwa na kijakazi wa nyumbani ambaye alimsaidia kwa shughuli za nyumbani. Zaidi ya hayo Bwana White alikuwa anamiliki bastola ambayo alikuwa ameificha chini ya mto (uk.85). Pia, kwenye gondoro la Bwana White alihifadhi shilingi laki sita. Mambo haya ni dhihirisho kuwa familia ya Bwana White lilikuwa ya tabaka la matajiri.

Mwandishi pia ametuchorea mandhari ya nyumbani kwa mhusika Farida. Katika mandhari haya, mwandishi ametuwezesha kutambua mhusika Juliet ambaye alikuwa msaidizi wa Farida nyumbani. Juliet anadhihirisha ujumbe wa mateso wanayopitia wanawake kutokana na mila na tamaduni za jamii. Jamii ya mama Juliet iliamini kuwa ndoa imekamilika kwa wanandoa kubarikiwa kupata mtoto. Mhusika Juliet anateswa na familia ya mumewe baada ya kukosa kujaliwa na mtoto. Jambo la kukosa mtoto lilisababisha Juliet kufukuzwa na kusutwa kuwa anajaza choo bure, yaani hana umuhimu wowote katika jamii hiyo (uk.163).

Mandhari haya ya nyumbani yanadhihirisha vile mwanamke aliyekosa mtoto alionekana kama binadamu asiyestahili katika jamii. Zaidi ya hayo, mandhari haya ya nyumbani yanatusaidia kutambua kuwa Juliet alidhulumiwa kimapenzi alipokuwa anafanya kazi kwa Mhindi kabla ya kupata kazi kwa Farida. Mwandishi anatudokezea kuwa Juliet akiwa jikoni Bwana Mhindi alipita akimshika mwili huku anajifanya anaangalia kitu fulani. Mkewe Mhindi mama Zarikha baada ya kutoka nyumbani, Bwana Mhindi anapata fursa ya kumpapasapapasa Juliet. Jambo hili linasababisha Juliet kuacha kazi kwa kudharauliwa na mwajiri wake na kutaka kumdhulumu kimapenzi:

> "... Baba mtu mpole. Juliet akiwa jikoni atapitia karibu akimshika
> mwilini huku akijifanya anaangalia kitu fulani jikoni, au atangojea
> kama mama hayuko ampapasepapase. Mwanamume gani huyu?
> Juliet alishindwa naye kwani amezuiliwa na nani kulisema alitakalo?
> Juliet alishindwakupapaswa na mtu tajiri yake. Si rafiki. Si
> mwafrika…" uk.163.

Bila shaka, mandhari hayo ya nyumbani yanadhihirisha tofauti iliyopo baina ya matabaka mbalimbali yaliyokuwa yakiishi katika jamii ya mwandishi. Tabaka la chini liliishi katika mandhari ya kutamausha ilhali tabaka la juu liliishi maisha ya starehe.

#### 4.1.1.2 Mandhari ya Chuoni

Mwandishi ametumia mandhari ya chuoni katika sehemu kadha wa kadha katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Jamii ya *Maisha Kitendawili* inachukulia swala la elimu kwa uzito, kwa kuwa kuna wale waliosoma hadi chuo kikuu kama Farida, Rose, Mary, Amos na Juma. Wote wanadhihirisha uhodari wao katika elimu. Rose anafanya vizuri masomoni kiasi cha kupewa tuzo la juu na Chuo Kikuu cha Mzalendo. Wahadhiri wanampongeza na kumpenda kwa matokeo mazuri. Pia mwandishi amedhihirisha jinsi sherehe ya kufuzu kwa mahafali

chuoni Mzalendo yalivyoandaliwa katika uwanja wa chuo sehemu iliyojulikana kama Biko Square (uk.73). Uwanja ulijaa umati kushuhudia wanaofuzu. Kujaa kwa uwanja huu wa Biko Square ni ishara ya kuwa jamii ya *Maisha Kitendawili* ilithamini elimu.

Mandhari haya ya Chuo cha Mzalendo yanatufichulia mbinu mbalimbali zilizotumika na wanafunzi katika kufanya mitihani yao. Kwanza kuna wanafunzi waliotumia mijadala kabla ya mitihani. Wahusika Rose, Juma na Amos wanathamini umuhimu wa mijadala kabla ya kufanya mitihani. Wanashirikiana pamoja katika mijadala.

Kuna wanafunzi ambao wanatumia mbinu za mkato ili waweze kufaulu katika mitihani yao. Mbinu hizi za mkato ni: wanafunzi kuwa katika makundi ya watu watatu watatu, kusoma mada fulani na wakati wa mtihani wanabadilishana karatasi na kunukuu majibu. Wengine waliandika nambari kwenye karatasi bila kuandika chochote na baada ya mtihani wanaondoka na karatasi ili mwalimu mwenye kusimamia mtihani alazimike kueleza kuhusu kutoweka kwa karatasi ya majibu ya mhusika. Mbinu nyingine ni kuwa asubuhi yake ya mtihani wangeandika kwenye mapaja majibu ya maswali wanayodhania yangekuwa (uk.51). Mbinu hizi zinafichua ujumbe wa udanganyifu katika mitihani.

Mandhari haya ya chuoni pia yametumika kufichua uozo unaofanyika chuoni kwa ajili ya wanafunzi kufaulu mtihani. Mwandishi ametumia mhusika Farida kuonyesha uozo huo. Farida anafichua hawezi kuanguka mtihani wa "supplementary" kwa kuwa anayesahihisha ni mwalimu Manoah na watazungumza kwanza kabla ya mtihani (uk.52). Jambo hili la mwalimu Manoah kuzungumza kwanza na Farida kabla ya kuufanya mtihani ni ishara ya udanganyifu katika elimu unaotendeka chuoni.

Matumaini ya kila mwanafunzi baada ya kufuzu ni kupata kazi. Kila mmoja aliyehutubu siku ya kufuzu chuoni Mzalendo aliwapa matumaini waliofuzu kuwa kila mmoja angepata kazi katika idara mbalimbali za serikali. Baada ya mkuu wa chuo Profesa Omar kuhutubia waliofika, mahafali na waliofika kushuhudia watoto wao wakifuzu sherehe ilifika kikomo. Wahusika Farida, Juma, Rose na Mary waliandaa sherehe ya kusherehekea kufaulu kwao masomoni. Sherehe iliandaliwa katika hoteli ya kifahari iliyoitwa Five Star Hotel International. Mhusika Juma anamdadisi Rose iwapo amepata kazi, kwa kuwa alisifiwa sana chuoni kwa kutia bidii. Rose anamdhihirishiaJuma kuwa yote yanategemea uhusiano wa mtu na wenye nguvu (uk.77). Jambo hili lilidhihirisha kuwa wanafunzi wengi baada ya kujikaza kwenye masomo na kufuzu kikwazo kikubwa ni kupata kazi. Wale wanaopata kazi ni wale ambao wanajuana na wenye mamlaka. Kupitia mandhari hayo tunapata ujumbe wa ufisadi unaoendelezwa katika jamii.

#### 4.1.1.3 Mandhari ya Kanisani

Mwandishi ametumia mandhari ya kanisani kuonyesha unafiki unaoendelezwa na viongozi wa kanisa pamoja na waumini. Mwandishi anatumia mandhari ya kanisani kupitia mhusika Rose kuonyesha mtu mnafiki aingiapo kanisani. Rose aliongoza nyimbo kanisani kwa sauti ambayo waumini walikiri kwamba ana kipawa cha kuimba. Siku ya Jumapili Rose aliingia kanisani akapiga magoti, akaanza kusali na kutikisa kichwa kama ambaye amebarikiwa na kipawa cha utambuzi wa Roho Mtakatifu (uk. 56). Kanisa limetumika kama mahali pa maficho baada ya waumini kutenda maovu. Rose anapoingia kanisani anajitambulisha kama mtu anayetii amri za Mungu, ilhali yeye ni mtu anayeshiriki usherati na uavyaji mimba. Mwandishi anatudokezea kuwa Rose tayari ametungwa mimba mara nne na kuwatupa watoto pipani. Pia Rose akiwa kanisani anadai kuwa Yesu ameshinda matendo

maovu kama uchawi, umalaya, mauti, wizi, uchoyo na uongo (uk.50). Matendo haya, mhusika Rose alikuwa anayatenda na yalikuwa kinyume cha amri za Mungu zinazosema:

> Biblia; Kutoka (20:13-17) usiue, usizini, usiibe na usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako.

Mandhari ya kanisani pia yamedhihirika katika kanisa la Msalaba Mweusi. Kupitia mhusika Kasu na Mjomba tunapata picha halisi ya kanisa hili. Familia ya Kasu ilimshawishi Farida na kumpeleka katika kanisa la Msalaba Mweusi. Mandhari haya ya kanisa yanashtua Farida.Kanisa hili liko katika hali mbaya. Watu wanaweza kuona ndani wakiwa nje, mlangoni kuna kinyesi cha mbwa. Pia mlango wenyewe unafunguka kwa shida kwa kuwa kanisa lenyewe limeinama na liko tayari kuanguka wakati wowote ule. Viambaza vya kanisa vimedondoka udongo wake. Jambo hili linadhihirisha unafiki. Kiongozi wa kanisa la mwombaji wa dini ya Msalaba Mweusi badala ya kulikarabati kanisa liwe katika hali nzuri anafuja pesa za waumini. Kiongozi huyu anatumia dini kujinufaisha kutoka kwa watu wanaofika katika kanisa hili. Licha ya kuwapora watu na kushindwa kulikarabati linabakia kuwa na matatizo mengi. Jambo hili linaonyesha unafiki wa kidini unaoendelezwa na viongozi wa kidini.

Kanisa la Msalaba Mweusi licha ya kuwa katika hali mbaya, mwandishi anaonyesha limekuwa kimbilio la wengi. Kila mmoja katika jamii ile anayekumbana na shida tofauti awe tajiri au maskini anakimbilia kwenye kanisa hilo kupata suluhu. Kuna baadhi wanaomini kuwa matatizo ya ndoa yanaweza kupata suluhu kutoka kanisa hili. Mambo haya ni dhihirisho kuwa mandhari haya ya kanisani yanatumika kuendeleza uozo na unafiki unaotendeka katika jamii na kutumia kanisa kuwahadaa waumini.

#### 4.1.1.4 Mandhari ya Hospitalini

Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia mandhari ya hospitalini kutoa picha halisi ya huduma za afya. Kwanza wahudumu wa hospitali hufika kazini wamechelewa, ukosefu wa maadili na upuuzaji wa baadhi ya madaktari, ukosefu wa dawa na mazingira machafu ya hospitali. Bwana Omar na mkewe Kibibi walikuwa wamefika hospitali kwa ajili ya kupata matibabu. Kupitia wahusika hawa tunapata picha halisi ya hospitalini. Kibibi na mumewe ndio walikuwa wa kwanza kufika hospitalini. Wahudumu wa hospitali hawakuwa wamefika. Kwa hivyo ilibidi wakae kwenye ubao uliokuwa unatumika kama kiti pale hospitalini. Polepole wagonjwa walianza kufika kwa ajili ya kupata matibabu na ubao uliotumika kama kiti ukajaa (uk.35). Mwanamke mmoja aliyezidiwa na maradhi alifika ila akapata ubao umejaa na hapakuwa na nafasi ya kukaa. Jambo hili lilisababisha mgonjwa huyu kulazimika kukaa sakafuni ambapo palikuwa na matope. Mwandishi anaelezea kuwa sakafuni hiyo haijapigwa deki kwa siku kadhaa. Jambo hili linadhihirisha kuwa utawala wa hospitali haukuwajibika katika kutekeleza majukumu yao.

Pia baada ya daktari kufika akiwa amechelewa kwa kuwa wagonjwa walikuwa wamefurika pale hospitalini, anasema ataanza na wagonjwa waliofika wa kwanza. Daktari hakujali kushughulikia mgonjwa aliyezidiwa na ugonjwa kwanza. Mgonjwa huyu anajinyoosha pale sakafuni hadi anaaga dunia. Bila moyo wa utu daktari anatoka ndani ya ofisi na kumwangalia jinsi alivyonyooka pale chini (uk.36).

Mandhari haya ya hospitali yanatoa picha halisi ya mateso wanayoyapiata wagonjwa wanapotafuta matibabu. Mateso haya ni kama kufika hospitali na kupata bado wahudumu wa hospitali hawajafika. Pia utepetevu wa wahudumu wa hospitali unadhihirika, kwa kuwa

sakafu ilikuwa chafu, mandhari haya yanastahili kuwa safi kwani ndiko wagonjwa hupata matibabu. Isitoshe, mandhari haya yanadhihirisha jamii ambayo haina utu na ambayo inadunisha mwanamke. Hili linadhihirika pale ambapo mgonjwa aliyefika hospitali akiwa amezidiwaalikuwa mwanamke. Wale waliofika na kukaa kwenye ubao wa hospitali hawakumwonea huruma na kumpisha aketi kwenye ubao. Mwanamke huyu aliketi sakafuni. Daktari baada ya kuwasili, badala ya kumpa huduma ya kwanza ili kuokoa maisha yake, anasisitiza ataanza nawale waliofika mapema. Ugonjwa unapomzidi mwanamke huyu anafariki bila kupata matibabu. Jambo hili linadhihirisha mapuuza ya baadhi ya madaktari.

Vilevile, mandhari hayo ya hospitali yanasaidia kutambua ujumbe wa ushirikina. Kupitia mhusika Bwana Omar tunatambua kuwa baada ya kutibiwa hakuridhika na matibabu hayo. Bwana Omar anaamini kuwa jambo ambalo linamsumbua ni mashetani(uk.36). Hili lilisababisha familia ya Bwana Omar kutafuta matibabu kwa mganga wa kienyeji anayejulikana kama Kalulu.

#### 4.1.1.5 Mandhari ya Ugangani

Mandhari haya yamedhihirika pale ambapo Bwana Omar na mkewe Kibibi walipokata shauri na kumtembelea mganga Kalulu. Mwandishi anatoa picha halisi ya mandhari ya Mganga Kalulu yalivyokuwa. Kwanza nyumba yake ilikuwa ndogo kwa hivyo ilibidi anayeingia ndanikupiga magoti au asote mpaka ndani (uk.37). Kwenye mlango kulikuwa na maua ya kila aina. Ndani mlikuwa na chupa za kijani, nyekundu, nyeupe zenye midomo mipana na miembamba. Vibuyu vilining’inia ukutani. Kwenye meza kulikuwa fuvu la kichwa cha mtu. Wakati wa kuhudumiwa wa Bwana Omar uliwadia. Bwana Omar anatapeliwa na kudhulumiwa na mganga Kalulu. Bwana Omar anashauriwa na mganga

Kalulu kutia shilingi moja katika kibuyu kisha mwenyewe kukizungumzia. Bwana Omar anatapeliwa kiuchumi na mganga Kalulu. Familia ya Bwana Omar ilikuwa maskini kwa kuwa haikuwa na pesa za kutosha kupata matibabu hospitalini. Zaidi ya hayo mganga Kalulu anadai gunia la korosho, mchele madebe mawili na damu ya mnyama. Kibibi alijizatiti kutafuta bidhaa hizi ila kwa matatizo mengi. Yeye ndiye aliyechukua majukumu ya kutunza familia baada ya Bwana Omar kuwa mgonjwa. Kibibi ndiye aliyewalea watoto wake Farida na Kasu.Jambo hili lilisababisha Kibibi kupitia hali ngumu kwa kujizatiti kutimiza maagizo ya Bwana Kalulu. Familia hii inapoteza mali kwa kutapeliwa mali yao na hatimaye Bwana Omar alifariki. Kupitia mandhari haya ujumbe wa ushirikina na ulaghai wa waganga unatambulika.

#### 4.1.1.6 Mandhari ya Mjini

Mwandishi ametuchorea mandhari ya mji wa Soweto. Kupitia wahusika Kasu na Yasmini tunapata picha halisi ya mji wa Soweto. Kasu na Yasmini baada ya kukamilisha masomo yao, wanaenda mjini kutafuta riziki. Katika mji wa Soweto mambo kadhaa yanatendeka. Kwanza Yasmini na Kasu wanafanya biashara ya ukahaba ili wapate hela za kulipa kodi. Pia vituko mbalimbali vilifanyika. Watu na wake zao kupigana katika vyumba jirani, watu kuomba kwa makelele, watu kuwasha stovu zenye makelele na wengine kuwaporomoshea wenzao madongo mchana na usiku (uk.26). Isitoshe, mandhari haya yanawasilisha ujumbe wa umaskini. Mwandishi anatudokezea kuwa mhusika Yasmini alitumia kamisi kufunga kitambaa cha pazia na kamisi hiyo ndiyo aliyotumia kufunika kichwa na pia kujisitiri. Jambo hili ni dhihirisho kuwa Yasmini hakuwa na uwezo wa kununua mavazi mazuri. Mambo haya ni dhihirisho kuwa watu walioishi katika mji wa Soweto ni watabaka la chini.

Pia uozo wa jamii unaendelea kudhihirika katika mji huu. Mhusika Kasu anakumbana na jibwa lililokuwa limebeba mtoto mchanga. Hii ni ishara ya kwamba baadhi ya watu katika jamii husika waliavya mimba na kurusha vijusi hivyo pipani. Baada ya Kasu kumwarifu Yasmini kuhusu jibwa hilo Yasmini anamweleza Kasu kuwa hayo mambo ya kuavya mimba ni tele Soweto: "…Leo mtu ana mimba kesho hana. Hana mtoto. Yuko wapi? Hana. Mara yuko pipani analiwa na mbwa…" (uk. 28).

Mandhari haya ya mji wa Soweto pia yanadhihirisha swala la utamaduni. Midundo ya ngoma ilisikika kwa mbali kisha ikaanza kukaribia. Ngoma, manyanga na kayamba zilisikika (uk.29). Wacheza ngoma hawa walipakwa matope na walicheza uchi. Walipokaribia, Kasu alimwuliza shaibu mmoja pale Soweto wale walikuwa akina nani? Hapa Soweto kuna watu wa asili tofauti. Kila kundi linafanya mambo kulingana na mila yake:

> "...Midundo ya ngoma iliyosikika kwa mbali ilianza kukaribia.
> Licha ya ngoma kulisikika manyanga na kayamba vilevile.
> Mara kundi la watu lilitokeazea likibenua kwa mabega, viuno,
> shingo na viungo. Walikuwa wakicheza uchi na ulikuwahuwezi
> kuwatambua. Mikononi mwao walikuwa na fimbo. Hapa Soweto
> kuna watu wa asili tofauti. Kila kundi linafanya mambo kulingana na
> mila yake. Hili hapa ni kundi la Wagisu ambalo linatayarisha vijana
> kwa tohara…" (uk. 30).

Jambo hili linadhihirisha mila na tamaduni za jamii ambazo zilidumishwa katika jamii ya mwandishi.

### 4.1.2.0 Mandhari ya Hali

Mandhari ya hali huonyesha namna jambo au shughuli ilivyofanyika. Hali hizi zinaweza kuwa za furaha au huzuni. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* mwandishi ametumia mandhari ya hali kuonyesha mambo ambayo jamii husika ilikumbana nayo.

### 4.1.2.1 Mandhari ya Mazishini

Mwandishi alitumia mandhari ya mazishi kuonyesha hali mbalimbali walizopitia wanajamii. Mandhari haya yanadhihirika katika mazishi ya marehemu Omar na Bi. Kibibi. Kibibi aliomboleza usiku na mchana. Mkojo ulimtoka Kibibi ovyo, makamasi yalimning'inia na akajigaragaza chini kama wazimu (uk. 40). Jambo hili linadhihirisha kuwa Kibibi alikuwa katika hali ya huzuni. Hali hii ya kuomboleza ilifanya Kibibi pia kufariki. Watu wengine waliranda mji mzima kwa huzuni na vilio na nyasi hazingeweza kuonekana popote. Jambo hili lilidhihirisha ushirikiano wa jamii wakati wa majanga. Matanga yalimalizwa kwa mazishi ya Bwana Omar na Kibibi. Mwandishi anatudokezea kuwa siku ya mazishi, Chifu wa lokesheni ya Mwasoko alipewa nafasi ya kuhutubia watu. Ilikuwa si kawaida watu wa namna hii kuzungumza katika mazishi maana wengi walidai eti ilikuwa ni kuhitilafiana na utaratibu wa kiitikadi (uk.41). Mandhari haya yanadhihirisha udumishaji wa mila na tamaduni za jamii ambazo zilistahili kufuatwa kwani wanajamii walihofia kutofuata mila zao kungesababisha jambo baya.

Mandhari haya ya mazishini yanadhihirisha kutoelewana kwa wanandoa. Baada ya matanga kukamilika, Farida na nduguye Kasu wanaenda kuishi na mjomba wao Bwana Marufuku. Jambo hili linasababisha Bwana Marufuku kutofautiana na mke wake. Bi. Marufuku alikasirika alipowaona Farida na Kasu wamekaribishwa nyumbani. "Basi kachukue mayatima wote ulimwenguni uwaangalie wewe''(uk.43). Jambo hili linasababisha Bwana Marufuku kunyimwa tendo la ndoa na mkewe. Mandhari haya

yanadhihirisha dhuluma alizopitia Bwana Marufuku kwa mkewe na pia dhuluma kwa Kasu kunajisiwa na mjomba.

> "…Ingawa mzee Marufuku alikuwa amewakaribisha wapweze Nyumbani kwa furaha, alizidi kuteswa na mkewe. Mkewe alimpokonya malazi. Alipoyauliza kama haki yake akaambiwa "Ngo". Hali hii ilimtia unyama Marufuku hadi akafikiria hatua ya kumnajisi Kasu..." (uk.44).

Mandhari haya yalijitokeza tena katika chumba cha kuhifadhi wafu. Mandhari haya ya mochari yalijitokeza pale ambapo Farida aliombwa na jirani yake kuandamana naye ili kuuchukua mwili wa marehemu Julia. Familia hiyo ilikuwa katika hali ya majonzi ila wakakumbana na mambo kadhaa ufuoni. Kwanza ufuoni kulikuwa na harufu ambayo iliashiria kitu ambacho kimeoza. Pia ndani kulikuwa na mvuke wa damu mbichi iliyotanda kila mahali (uk.153). Miili ya wafu ilitapakaa kila mahali kwenye sakafu. Pili familia ya marehemu Julia inapewa mwili wa marehemu na wahudumu wa mochari baada ya kupewa hongo. Mwandishi ametumia mandhari haya kuwasilisha ujumbe wa ufisadi ambao unaendelezwa katika mochari bila kuhurumia jamii iliyompoteza mtu wao.

#### 4.1.2.2 Mandhari ya Afya

Mwandishi anaeleza hali ya afya ya jamaa mashambani. Kupitia wahusika mbalimbali mwandishi amedhihirisha hali walizopitia wanajamii katika kuwatuza wagonjwa wao. Familia yaBwana Omar ilikuwa imezowea hali ya ugonjwa wa pumu kwani alizaliwa akiwa na ugonjwa huu mgonjwa. Mwandishi anatudokezea kuwa Bwana Omar alipokuwa mtoto, vijana wenzake walimbandika majina kwa ajili ya ugonjwa wa pumu (uk.32). Hali hii ilimfanya mkewe Bwana Omar kuchukua jukumu la kumtunza mumewe. Kibibi alijifunza kuvumilia hali hii na kuchukua jukumu la kumwangalia na kumshughulikia. Bi

Kibibi alifanya kazi ya ukulima ili kutimiza mahitaji ya familia. Mapato aliyopata ndiyo aliyoshughulikia Bwana Omar na watoto wake Farida na Kasu.Kifo cha Bwana Omar kilichotokea baada ya kuzidiwa na ugonjwa kinasababisha hali ya huzuni katika familia. Hali hii ya huzuni inasababisha Bi. Kibibi kuaga dunia baada ya kuomboleza kwa siku kadhaa. Jambo hii inadhihirisha hofu na huzuni katika ndoa.

Familia ya Mama Josii ni familia nyingine ambayo inajizatiti kutunza familia licha ya bwanake kuwa mgonjwa kwa miaka saba. Mama Josii alijitwika jukumu la kumtunza mumewe na pia watoto wake ambao walikuwa wengi (uk. 68). Ingawa familia hii iliishi katika nyumba iliyovuja ukutani na paani, Mama Josii alihakikisha kuwa mumewe na watoto wake wamepata chakula cha kila siku.

Mandhari haya yanadhihirisha hali mbalimbali. Yanadhihirisha swala la uvumilivu katika ndoa. Familia ya Bwana Omar na familia ya Mama Josii ilipitia hali ngumu ya maisha. Licha ya familia hizi kupitia changamoto nyingi katika kuyatibu magonjwa yaliyowapata bwana zao na kuwatafutia lishe bora, walivumilia changamoto hizo. Mwandishi ametumia wahusika wa kike kuonyesha kubadilika kwa utamaduni wa Kiafrika kuhusu majukumu ya kulea familia. Jukumu la kuitunza familia mara nyingi huachiwa mwanaume. Kupitia wahusika Kibibi na Mama Josii ni dhahiri kuwa jinsia ya kike ndiyo iliyoachiwa jukumu la kutunza familia. Kwa kuwa hali ya ugonjwa ilikuwa imewalemea Bwana Omar na mumewe Mama Josii hawakuwa na nguvu za kutekeleza majukumu ya familia.

Kupitia aina mbalimbali za mandhari ambazo zimedhihirika katika riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika,* ni dhahirikuwa mandhari hayo ni halisi. Nadharia ya uhalisia husisitiza kuwa katika kazi ya fasihi mwandishi hana budi kutumia mandhari halisi ambayo

yanadhihirisha ukweli wa maisha. Habwe ametumia mandhari halisi kama mandhari ya nyumbani, kanisani, shuleni, mjini, mazishini na mandhari ya usiku. Kwa hivyo, mandhari haya ni halisi si ya kinjozi.

## 4.2 MANDHARI YALIVYOSAWIRIWA KATIKA *ROSA MISTIKA*

### 4.2.0 Utangulizi

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mandhari ya aina mbalimbali yametumika kwa ajili ya kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Mara nyingi wanafasihi wanaathiriwa na mambo yanayotendeka katika jamii yake. Katika hali ya ubunifu mwandishi anasawiri matukio katika wakati, hali na mahali fulani. Kwa hivyo, mandhari katika riwaya ya *Rosa Mistika* nimeyainisha katika aina tatu. Mandhari ya mahali, mandhari ya wakati na mandhari ya hali.

### 4.2.1Mandhari ya Mahali

Mandhari ya mahali huelezea ni wapi tukio hutokea. Kila kisa katika fasihi huwa na sehemu tofauti na huwa na mandhari tofauti. Mahali pa upekee panaweza kutumiwa kutoa asili ya mgogoro mpya. Pia mandhari ya mahali yanaweza yakahusu dunia, nchi, jiji, mji,kijiji, kitongoji na hata ndani ya nyumba. Mandhari ya mahali katika riwaya ya *Rosa Mistika* yanajitokeza pale ambapo mwandishi anaendeleza wahusika wake ili kufanikisha ujumbe wake. Mandhari haya yanadhihirika kwa njia mbalimbali.

#### 4.2.1.1 Mandhari ya Nyumbani

Mwandishi ametuchorea mandhari ya nyumbani katika sehemu mbalimbali. Kwanza nyumbani kwa mhusika Rosa. Mwandishi anatuonyesha mandhari ya taabu ambazo mhusika Rosa na familia yao walipitia. Nyumba yao ilikuwa mbovu na ilivuja wakati wa mvua:

> "…Usiku huo mvua ilinyesha kwa wingi sana. Lo! Nyumba ilikuwa kama mti, ilivuja kustaajabisha. Kulikuwa na ngozi za ng'ombe mle ndani ya nyumba. Regina alizichukua na kuwafunika watoto wake…" (uk. 13).

Mandhari haya yanatuonyesha tabaka la mhusika Rosa na familia yake. Hii ni familia iliyo katika tabaka la chini ambayo iliishi katika nyumba duni. Ubovu wa nyumba yao, nyumba iliyokuwa imelala upande, iliyovuja maji kama mti, pia katika nyumba hiyo wahusika Rosa na dada zake walijifunika matandiko ya ngozi ya ng'ombe. Jambo hili lilidhihirisha wazi kuwa familia ya Bwana Zakaria ilikuwa ya tabaka la chini. Mandhari haya ya nyumbani kwa mhusika Zakaria yametoa picha halisi ya nyumba yake na jinsi walivyoishi katika lindi la umaskini.

Kupitia mandhari ya nyumbani kwa Bwana Zakaria tunapata picha halisi, jinsi Bwana Zakaria alivyowadhulumu watoto wake pamoja na mke wake Regina. Bwana Zakaria kila akilewa na kurudi nyumbani usiku, alimwamsha mkewe pamoja na watoto wake. Bwana Zakaria aliwalazimisha watoto wake kuimba nyimbo usiku huo. Ni katika mandhari haya tunafahamu jinsi Bwana Zakaria alivyodhibiti mhusika Rosa. Baada ya Bwana Zakaria kupata habari kuhusu barua aliyoandikiwa Rosa na Charles. Bwana Zakaria anachafuka roho na kumpiga Rosa hadi damu ikamtoka. Jambo hili linamlazimu Bwana Zakaria kuandamana na Rosa hadi nyumbani kwa Bwana Ndalo ambako Charles aliishi (uk.4-6).

Mandhari ya nyumbani pia yanajitokeza kwa mhusika Bwana Ndalo. Regina baada ya kumpikia uji mumewe Bwana Zakaria, anakata shauri na kuelekea nyumbani kwa Bwana Ndalo ili kufanya upelelezi zaidi kuhusu jinsi Zakaria alilewa jana (uk.17). Ni katika

mandhari haya ya nyumbani kwa Bwana Ndalo ambako swala la imani zisizokuwa na mashiko zinaibuka. Ndalo na Bi Bigeyo walikuwa wanakula nyama ya kuku huku wakikimbia kuizunguka nyumba. Jambo hili linadhihirisha kuwa familia ya Bwana Ndalo iliamini kuwa ilikosa kufanikiwa kupata mtoto kwa sababu ya tamaduni za jamii yao. Bi Bigeyo alikuwa hazai kwa sababu alipokuwa msichana alikataa kuwabeba wadogo zake mgongoni. Mandhari haya yametumika kufanikisha ujumbe wa imani potovu za jamii ya mwandishi ambazo zimepitwa na wakati. Imani hizi hazidhaminiwi na jamii ya kisasa na zinachukuliwa kuwa ushirikina.

**4.2.1.2 Mandhari ya Shuleni**

Mwandishi ametumia mandhari ya shule katika sehemu kadha wa kadha katika riwaya ya *RosaMistika*. Kwanza anatuonyesha vile mandhari ya mhusika Rosa yalikuwa akisoma shule moja na Charles ambayo ilijulikana kama Murutunguru Upper Primary School (uk.7). Mhusika Charles alikuwa anaishi kwa mjomba wake Bwana Ndalo, kwa kuwa kwao kulikuwa mbali na shule ambayo angesomea. Mandhari haya ya shuleni yanawafanya Charles na Rosa kushirikiana kwa kuwa walisoma darasa moja. Isitoshe, kila siku walienda shuleni pamoja na kila jioni walirudi pamoja. Jambo hili lilisababisha Charles na Rosa kuwa wapenzi. Hili linadhihirika kupitia kwa barua aliyoandika Charles kwa Rosa:

> Mpenzi Rosa Mistika
> “Ewe ua waridi lenye fumbo! Ewe dada wa makao yangu uliye kitulizo changu! Funua macho uione makala hii fupi ya mapenzi nakuota kila siku wakati wa usiku, sipati usingizi kwa ajili yako. Kuvumilia nimeshindwa. Tafadhali unijibu upesi. Nakutakia ushindi mzuri katika mtihani wako.”
> Wako katika mapenzi na matumaini, Charles Lusato (uk.8).

Mandhari hayo ya shule ya msingi yalichangia wahusika Charles na Rosa kuwa wapenzi. Mandhari ya shule ya upili ya Rosary yalikuwa ya kijazanda. Shule hii ilikuwa imejengwa kupakana na barabara. Pia ilikuwa na milima kila upande, na milima ilijaa mawe makubwa meusi na mapango ambamo fisi walikuwa wakilala (uk.21). Mandhari haya yanadhihirisha kuwa wasichana wa shule ya Rosary walikuwa hatarini. Walihitaji kulindwa kutokana na mashambulizi ya wenzao kutoka shule jirani. Udhibiti huu unadhihirika kupitia mawe makubwa ambayo yana mapango yaliyokuwa na fisi. Wasichana waliosomea katika shule hii walikuwa wakidhibitiwa katika maeneo ya shule. Shule tano zaidi zilikuwa zimejengwa kwenye milima hii. Shule hizi zote zilikuwa za wavulana isipokuwa moja ilikuwa ya wasichana. Mandhari haya yanadhihirisha mambo mbalimbali. Kwanza shule hii ilihitaji ulinzi wa kutosha, kwa kuwa ilijengwa karibu na barabara. Pia ilikuwa ndiyo shule ya pekee ya wasichana kati ya shule tano za wavulana. Usalama wa wanafunzi katika shule ya Rosary ulithibitiwa kwa kuwa ilizingirwa na milima kila upande. Pia milima hiyo ilikuwa na mawe.

Shule ambayo mhusika Rosa alikuwa anajiunga nayo iliendeshwa na Sista (uk.21). Mwandishi anadhihirisha kuwa masista walifaa kuongoza shule hii kwani ilikuwa imejengwa kati ya mbwa mwitu. Isitoshe, mandhari haya yanazua ujumbe wa ufisadi. Ufisadi huu unadhihirika pale ambapo nafasi ya Rosa katika shule hii ilikuwa inapiganiwa na wengi. Afisa mmoja alikuwa amemwambia Sista kuwa Rosa alikuwa amekufa maji akiogelea ziwani ili kupata nafasi hiyo.

Mandhari haya ya shule ya Rosary yanaibua mambo yafuatayo. Kwanza kubadilika kwa mila na tamaduni za Kiafrika. Katika shule hii wanafunzi walikuwa na mpango wa kucheza dansi na wavulana kutoka shule mbalimbali mara tatu katika muhula (uk.22). Hii ni

kinyume na mila za Waafrika. Pia mandhari haya yanafichua sheria kali zilizowekwa katika shule hiyo. Mwanafunzi yeyote aliyepatikana amevunja sheria za shule alifukuzwa shuleni, mfano wasichana waliopatikana na hatia ya kuchoma vitabu na nguo za Rosa walipewa barua za kufukuzwa shuleni na huo ukawa mwisho wa masomo yao (uk.29).

Mandhari mengine ya shuleni yanajitokeza ni pale ambapo Rosa anamtembelea dadake Flora shuleni. Mwandishi anatuonyesha jinsi shule ya Flora ilizunguukwa kwa waya ya seng'eng'e na lango la shule lilikuwa mbali na shule. Pia lango lililindwa na polisi:

> "… alifika shuleni saa saba. Alishangaa kukuta mlango umefungwa na polisi alikuwa akiulinda. "shida!" Rosa alinyamaza." Njoo hapa!" polisi alimwita. Unataka kumwona nani? Dada yangu. Saa bado mpaka saa nane…" (uk.61).

Sheria katika shule hii zilifuatwa na kila mwanafunzi na yeyote aliyetembea shuleni. Kwanza polisi waliandika jina la Rosa katika daftari kabla ya kumruhusu kuingia. Pia mhusika Rosa ilikuwa lazima kumwona mwalimu wa zamu kabla ya kumwona dadake ili apewe ruhusa. Mhusika Rosa alikuwa lazima athibitishe kwamba Flora alikuwa dadake ndiposa apewe ruhusa ya kumwona. Mandhari haya yanadhihirisha kuwa vijana katika shule hii ya Katoliki wamedhibitiwa. Pia licha ya wasichana wa shule hii kudhibitiwa kuna wale ambao hupata mimba na kufukuzwa shuleni. Hii ni ishara kuwa licha ya sheria kali katika mandhari ya shule kuna wale waliotenda kinyume na sheria hizo.

Kupitia mhusika Rosa athari ya mandhari ya Chuoni cha Ualimu cha Morogoro kwa mhusika yanajitokeza. Katika chuo hiki mwandishi anadhihirisha yale mambo yaliyotendeka chuoni humo. Mhusika Rosa akiwa chuoni alipewa jina la utani "laboratory" (uk.45). Jina hili lilifichua vitendo vya Rosa kama kuavya mimba na pia kufanya uzinzi na

mwalimu mkuu wa chuo Bwana Thomas. Mandhari ya Chuo cha Ualimu cha Morogoro yanaonyesha jinsi mwandishi amechora mwanamke kama chombo cha starehe katika jamii yake. Pia mandhari hayo yamedhihirisha uozo unaotendeka katika jamii. Isitoshe, mandhari haya yanatufichulia jukumu la Padri katika chuo hicho. Padri baada ya kupata habari za mhusika Rosa alijaribu kumrekebisha Rosa kwa kumpa matumaini na wosia ufaao. Maneno ya Padri yaliambulia patupu. Rosa anamkemea Padri hadi Padri anatoweka na kumwacha Rosa peke yake:

> "… Rosa alianza kutapika maneno, "wokovu maana yake nini? Wokovu kama kuna moto basi nitaenda. Padri maisha yangu yamekwishaharibika na sijali." Padri alimwangalia Rosa akashangaa. Alisimama na kufungua mlango na kutoka…" (uk.49).

Mandhari ya chuoni yanafichua swala la ukabila. Baada ya Bwana Thomas kufumaniwa na mkewe akiwa na Rosa, ujumbe wa ukabila unafichuka. "Sijui kwa nini serikali ilikupa ukubwa, ulipata cheo hiki kwa sababu ya ukabila." (uk.54). Kwa hivyo inaonyesha Bwana Thomas hakuwa na elimu ya kumfanya kuwa Mkuu wa Chuo bali alipewa cheo hicho katika misingi ya ukabila.

#### 4.2.1.3 Mandhari ya Baa

Mwandishi ametumia mandhari ya baa ambako wasichana wa shule ya Rosary walienda kunywa pombe na kucheza densi. Katika mandhari hayo Rosa anapata rafiki mgeni aliyejulikana kama Deogratias na kucheza naye densi. Bila mandhari hayo, Rosa hangekutana na Bwana Deogratias ambaye alifanya Rosa kuishiwa na fahamu. Mapenzi ya Rosa na Bwana Deogratias yalifanya Rosa kubadili tabia na kuanza kufeli mitihani. Jambo hili lilisababisha Rosa kufukuzwa shuleni (uk. 35).

Mhusika Rosa alipokuwa mjini Mwanza, baada ya kusikia habari za mchumba wake Deogratias, aliamua kwenda baa kujifurahisha ndiposa kusahau msiba alioupata wa kutengwa na Deogratias. Rosa alipoingia "Green Bar", humo ndani aliona mengi. Ujanja wa wanawake na ujinga wa wanaume, unyonyaji wa wanawake na unyonywaji wa wanaume. Mandhari hayo ya baa yametumiwa na mwandishi kuonyesha uozo unaotendeka katika jamii ya mwandishi. Uozo huu ni kama vijana kulewa wakiwa na umri mdogo, watu kutapeliwa na kuibiwa hela zao wakiwa wamelewa:

> "…sisi ni mali yenu tu, walijibu pamoja. Wale vijana waliyumbayumba kwenda zao kulala. Rosa anawaona wale wanawake wanapeana mikono wakicheka. "Heko mwenzangu, tumewatengeneza, tumetumia zaidi ya shilingi mia ishirini…" (uk.42).

#### 4.2.1.4 Mandhari ya Mjini

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika*ametumia mandhari ya mjini ambako Bwana Ndalo alikuwa anafanya kazi. Rosa na dadake Flora waliandamana hadi katika duka la Bata ambalo Bwana Ndalo alifanya kazi, kwa ajili ya kujiandaa kwenda shuleni. Ni katika mandhari haya Rosa alipata viatu alivyokuwa anataka ila kwa bei ghali. Rosa na dadake Flora walijaribu kumshawishi mwenye duka ambaye alikuwa Mhindi kupunguza bei hadi shilingi kumi na tisa bila mafanikio. Bwana Ndalo aliwaelekeza mahali ambapo wangepata kwa bei nafuu. Jambo hili lilisababisha Bwana Ndalo kufutwa kazi na kutukanwa na mwenye duka (uk.15). Bwana Ndalo anadhulumiwa kwa kutupwa nje na kurushiwa shilingi zake tano. Mandhari haya yanadhihirisha ujumbe wa utabaka. Watu wenye mali ndio wanamiliki maduka katika mji huu. Mwanabiashara Mhindi anauza vitu kwa bei ghali

kuliko maduka mengine. Jambo hili linasababisha wanajamii wa tabaka la chini kushindwa kununua bidhaa muhimu walizohitaji. Bwana Ndalo anadhulumiwa kwa kutukanwa na kufutwa kazi. Baada ya kufutwa kazi anapewa malipo duni ya shilingi tano. Pia mwandishi amefanikiwa kuonyesha jinsi wanajamii wanataabika kupata bidhaa muhimu katika mji huo kwa sababu ya hali yao ya mapato.

#### 4.2.3.0 Mandhari ya Wakati

Mandhari ya wakati hujibu swali la ni lini jambo fulani linatokea, lilitokea au litatokea. Wakati huu unaweza kuwa kipindi fulani. Pia wakati unaweza kuwa mchana ama usiku. Mandhari ya wakati hudhihirishwa na mabadiliko ya hali ya anga kama msimu wa masika au msimu wa kiangazi. Kipengele hiki cha wakati humwelekeza msomaji kuelewa nyakati palipotokea matukio fulani katika jamii husika. Mandhari ya usiku yanaashiria kipindi ambamo maovu huendelezwa. Ni kipindi ambacho kiza hugubika matendo ya binadamu na kumpatia ujasiri wa kushiriki maovu. Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mandhari ya wakati yametokea katika sehemu zifuatazo:

#### 4.2.3.1 Mandhari ya Usiku

Mandhari ya usiku yanajitokeza katika sehemu mbalimbali katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Mwandishi anatuonyesha jinsi Zakaria na bintiye Rosa walienda nyumbani kwa Bwana Ndalo usiku (uk.8). Hii ni baada ya Stella kumwarifu Bwana Zakaria kuwa Rosa aliandikiwa barua na Charles. Mwandishi anatuonyesha chumba alichokuwa amelala Charles. Charles alikuwa na kijumba kidogo cha majani (uk.7). Kijumba hiki kinadhihirisha kuwa familia ya Bwana Ndalo ilikuwa ya tabaka la chini, kwani hawakuwa na uwezo wa kujenga nyumba nzuri.

Mwandishi anaonyesha hali waliyokuwa Bwana Ndalo na mkewe. Walikuwa wamejifunga shuka zao na mwezi uliwang'aria na nyota ziling'aa, wote kushuhudia ukatili uliokuwa ukiendelea siku hiyo. Huu ni wakati Rosa alikuwa ameandikiwa barua na Charles. Kujifunga shuka kwa Bwana Ndalo, mkewe pamoja na Charles na mwezi kung'aa kuliashiria kuwa jambo hili lilifanyika wakati wa usiku.

Bwana Zakaria na mgeni wake Deogratias walienda kulewa wakati wa usiku. Kulewa huku kulifanya fujo kutokea na watu kuanza kukimbia kwa ajili ya kujiokoa. Kwa bahati mbaya kichaka chote kilikuwa kimezunguukwa na polisi, na Bwana Deogratias kutiwa mbaroni kwa kuwa hakujua maeneo hayo vizuri. Bwana Deogratias alipojaribu kujitetea alizabwa kofi mpaka akaanguka na kuzimwa kwa kiatu kifuani na tumboni. Damu ilimtoka puani. Walipokamatwa walipelekwa gerezani (uk.39). Mandhari haya ya usiku yanatufichulia dhuluma ambazo wanajamii hupitia mikononi mwa polisi nyakati za usiku wanapotiwa mbaroni. Pia yanatufichulia hali halisi ya gerezani na mazingira yao yalikuwa katika hali duni. Blanketi lilikuwa moja na lilikuwa limezeeka na pia walitumia ndoo moja kwenda haja na ilikuwa imejaa.

Mandhari ya usiku pia yametumika katika chumba cha mwalimu mkuu Bwana Thomas. Mhusika Rosa anamtembelea mpenziwe Bwana Thomas wakati wa usiku, pale ambapo wanafanya uzinzi. Jambo hili linasababisha Bwana Thomas na Rosa kufumaniwa na mkewe usiku wa manane. Jambo hili linazua ujumbe wa ukosefu wa uaminifu katika ndoa na uozo unaofanyika katika jamii husika (uk.54). Mandhari ya usiku, yanaonyesha uozo mwingi wa jamii hulifanyika usiku.

#### 4.2.4 Mandhari ya Hali

Mandhari ya hali huonyesha namna jambo au shughuli ilivyofanyika. Hali hizi zinawezekana kuwa za furaha au huzuni. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi ametumia mandhari ya hali kuonyesha hali ambazo jamii husika ilikumbana nazo.

##### 4.2.4.1 Mandhari ya Huzuni

Mwandishi alitumia mandhari ya huzuni kuonyesha hali mbalimbali walizopitia wanajamii. Mandhari haya yalidhihirika katika mazishi ya mwendazake Bwana Ndalo (uk.88). Bigeyo alikuwa amekaa karibu na maiti ya mumewe Bwana Ndalo. Mwandishi anatudokezea kuwa Bigeyo alikuwa katika hali ya huzuni. Alikuwa analia kwa sauti huku akimpapasa marehemu mumewe akisema, 'Mbona umeniacha.' Jambo hili linadhihirisha jinsi mapenzi ya Bigeyo yalikuwa kwa Bwanake Bwana Ndalo licha ya kukosa kubahatika kupata mtoto.

Mandhari hayo yanadhihirisha taratibu ambazo hufuatwa na jamii ya mwandishi wakati wa majonzi. Mwandishi anatudokezea kuwa katika hafla ya mazishi, taratibu fulani zilifutwa. Taratibu hizi ni baada ya kaburi kuwa tayari, maiti huoshwa na kutolewa nje kwa ajili ya watu waliofika kumpa heshima ya mwisho mwenda zake (uk.89).

Mandhari haya yalijitokeza tena katika mazishi ya Zakaria, Regina na Rosa (uk. 93). Katika mandhari haya mwandishi anaeleza kuwa vichwa vya maiti vilikuwa vimeachwa wazi ili watoto watazame wazazi wao mara ya mwisho. Mandhari haya ya kutazama nyuso za wendazake yaliibua maswala ya taratibu ambazo jamii ya mwandishi ilifuata wakati wa mazishi.

Katika mandhari haya ya huzuni swala la utani lilidhihirika. *Kamusi ya Fasihi na Nadharia* (2003), inafafanua kuwa utani ni dhana inayotumiwa kuelezea hali ya kufanyiana mizaha

miongoni mwa wanajamii au jamii mbalimbali bila ya kuogopa kushtakia. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), utani ni taratibu za kimila ambazo zinawafanya watu kuambiana au kutendeana jambo lolote bila ya chuki. Sengo na Lucas (1975), wanaeleza kuwa utani wa Kiafrika ni udugu mzito wenye isimu au chanzo chake kwenye matukio ya kimaisha. Wataalamu hawa wamehusisha utani na matukio yanayofanyika katika jamii kama matambiko. Zaidi ya hayo utani hufanywa kulingana na utamaduni na kaida za jamii inayohusika. Katika mazishi ya Bwana Ndalo, Bwana Zakaria alitania waombolezaji kwa kupiga kelele na kusimama juu ya kaburi la marehemu Ndalo (uk.89). Jambo hili lilisababisha Bwana Zakaria kufumwa mkuki kifuani hadi kufariki. Jamii ya Wakerewe illifanya utani kwa kufuata kaida ambazo ziliwekwa.

Utani mwingine ulidhihirika katika mazishi ya mwenda zake Zakaria, Regina na Rosa. Baada ya Padri kukamilisha shughuli zake mtu mmoja alipiga kelele na kufanya utani. “Nimemletea Zakaria chupa mbili za moshi.” Alichukuwa chupa moja na kuitupa kaburini. Mtu huyo alitiwa mbaroni kwa kitendo hicho (uk.94). Mandhari haya yanadhihirisha kuwa utani katika jamii ya Ukerewe haukubaliki wakati watu wanaomboleza.

## 4.3 MCHANGO WA MANDHARI KATIKA KUWASILISHA UJUMBE

### 4.3.1 Utangulizi

Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* ameangazia mambo mengi ambayo anayaona katika jamii yake. Baadhi ya mambo haya ni utabaka unaodhihirika katika jamii, uvumilivu katika ndoa, dhuluma ambazo wanajamii wanapitia, utamaduni wa jamii katika kutelekeza mambo yao ya kila siku, thamani ya elimu, ufisadi na unafiki wa dini katika jamii ya mwandishi. Ujumbe huu wa mwandishi umefanikishwa kupitia mandhari mbalimbali kama mandhari ya nyumbani, mandhari ya chuoni, mandhari ya kanisani,

mandhari ya ugangani, mandhari ya mjini, mandhari ya hospitali na mandhari ya mazishini. Bila matumizi ya mandhari haya ujumbe wa mwandishi haungeeleweka kwa njia inayofaa. Sehemu hii imechunguza mchango wa mandhari hayo katika kuwasilisha ujumbe wa mwandishi.

### 4.3.2 Ujumbe katika riwaya *Maisha Kitendawili*

#### 4.3.2.1 Utabaka

Utabaka ni zao la utumwa, umwinyi na ubepari. Asili ya mifumo hii yote inatokana na njia za uzalishaji mali. Wanadamu walipodhiri duniani, waliishi kwa pamoja na udugu. Maisha haya ya kuishi pamoja yalizaa ujima. Katika mfumo wa ujima hakuna mtu binafsi aliyemiliki mali. Mali ilikuwa ya jamii yote na kila mmoja alikuwa na mchango katika uzalishaji mali. Watu walifanya kazi kwa pamoja na mazao yalimilikiwa na jamii yote na kila mmoja kufaidika. Hakuna yeyote aliyekuwa bwana wa kutuma na kutumikiwa. Watu walifanya kazi kwa ujima na kusaidiana (Senkoro,1987:18).

Kadri mwanadamu alivyoendelea, ujima ulianza kufifia na umoja wa ukabila ukaanza kubomolewa na ugawanyikaji wa kazi kuzuka. Jamii ikazua viongozi, miongoni mwao machifu na baraza la wazee. Machifu hawa wakaanza kujipa uwezo wa kuamua baadhi ya mambo. Wakawa wanaanza kupata zawadi mbalimbali na kuheshimiwa. Polepofle mbari zikaanza kubomoka katika harakati ya kuongoza machifu wakawa ndio wenye ardhi na matajiri. Hatimaye matajiri hawa wakaanza kununua watu na kuwatumikia watakavyo. Hivyo utumwa ukazuka na utabaka wa jamii ukaanza kudhihirika. Machifu na matajiri wakawa tabaka la juu nao watumwa wakawa tabaka la chini.

Matajiri walizidi kuwa matajiri zaidi na watu wachache ndio waliomiliki ardhi kubwa na kuwakodisha wasio matajiri kulima na kisha baadaye kutoa fungu kubwa sana kwa mwenye shamba wakati wa mavuno. Hali hii ikazaa umwinyi. Umwinyi huu ukaendeleza utabaka, kuwa na walionavyo (tabaka la juu) na wasiokuwa navyo (tabaka la chini).

Muda ulivyoendelea, umwinyi ukaboreka baada ya uvumbuzi wa teknolojia huko Ulaya na kuzaa upebari. Matajiri wakamiliki viwanda ili kuzalisha mali zaidi. Tabaka la juu likawa la wamiliki viwanda na tabaka la chini likawa wafanyikazi katika viwanda hivyo. Katika mfumo huu, kila kitu kikawa bidhaa na lazima kinunuliwe. Wamiliki viwanda wakawa matajiri zaidi na wafanyikazi wakanyanyaswa zaidi. Wakafanyishwa kazi nyingi kwa malipo duni. Mfumo huu humtukuza tajiri ambaye kwa kutumia uwezo wake au wa kiuchumi anapata atakacho kwa kuwanyanyasa wanyonge. Enzi hii ndiyo utabaka ulifika upeo, kukawa na watu wa tabaka la juu na tabaka la chini (Senkoro 1987).

Kwa hivyo, utabaka asili yake ni mandhari ya uzalishaji mali kuanzia utumwa, umwinyi na ubepari. Jamii nayo ikagawanyika dhahiri, matajiri wakawa na maeneo yao ya kifahari wanamoishi na maskini maeneo yao ya mitaa ya mabanda au nyumba duni. Jambo hili likazaa mandhari ya kitajiri na mandhari ya kimaskini. Watu wa tabaka la juu wakawa ni wale wanaomiliki mali, wanaishi maisha ya starehe, nyumba zao ni za kifahari, wanamiliki magari ya kifahari, wanalindwa mchana na usiku, chakula kwao si shida na pia wanawadhulumu wasiokuwa na mali. Nao maskini (tabaka la chini) waliishi kwenye maskani duni, ukosefu wa mavazi, ukosefu wa lishe bora, mishahara duni, ukosefu wa kazi na kukosa hela za kugharamia matibabu (Senkoro 1987).

Mtunzi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* amesawiri na kuwasilisha uhalisi wa utabaka katika jamii yake. Watu katika riwaya hii wamegawika katika matabaka mawili makuu. Tabaka la chini (maskini) na tabaka la juu (matajiri). Tabaka la chini ni la watu wasiokuwa na mali, wanaishi kwenye maskani duni, ukosefu wa lishe bora, ukosefu wa mavazi, mishahara duni na wanaokosa pesa za kugharamia matibabu. Tabaka la juu ni watu waliomiliki mali, wanaishi maisha ya starehe, nyumba zao ni za kifahari, wanamiliki magari ya kifahari, wanalindwa mchana na usiku, lishe kwao si shida na pia wana kiburi kinachowapelekea kudhulumu walio katika tabaka la chini. Mandhari mbalimbali yametumika kufanikisha ujumbe wa utabaka katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*.

Kwanza, mandhari ya mjini (uk. 25). Mwandishi ametumia mandhari ya mji wa Soweto kudhihirisha jamii iliyoishi katika hali ya uchochole. Kupitia wahusika Kasu na Yasmini mwandishi ameonyesha jinsi walivyopitia changamoto nyingi za maisha. Wakiwa mjini Soweto, chumba walichoishi mlangoni kulifunikwa kwa pazia iliyochanika. Pia pazia hiyo ilikuwa na vitone na ilikuwa imebadilika rangi na kuwa na rangi nyingi. Jambo hili linaashiria kuwa kazi walizofanya Kasu na Yasmini hazikuwa na mapato ambayo yangewawezesha kununua pazia nzuri.

Kasu na Yasmini walienda mji wa Soweto kutafuta maisha. Yaani walienda kutafuta kazi ambayo ingewapa pesa za kujikimu kimaisha. Baada ya kukosa kazi walifanya biashara ya ukahaba. Walishiriki katika ngono kwa malipo ili waweze kupata pesa za kulipa kodi ya nyumba na pia kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Hali ya maisha mjini Soweto ilikuwa ya chini. Hili linadhihirika kupitia nyumba za mabanda. Vibanda hivi vilijengwa kwenye mteremko mkali ajabu. Watu walioishi katika vibanda hivi walikuwa wanafanya mambo

ya ajabu kama, watu na wake zao kupigana kila mara, watu kuomba kwa makelele na watu kuwasha stovu zenye kelele.

Pia mji huo wa Soweto haukuisha vituko vya kutisha kama watoto kutupwa kwenye mapipa ya taka (uk. 27). Yasmini kuamshwa na Kasu kuliona jibwa lililobeba mtoto mdomoni. Mwandishi anatudokezea kuwa Yasmini baada ya kuamshwa na Kasu alichukua kamisi kwenye kamba ya mkonge ambayo ilitumiwa mchana kufunga kitambaa cha pazia. Pia baada ya kuivaa kichwani aliivuta kufunika sehemu ya chini ambako alikuwa kavaa nguo ya ndani iliyochanika na kupoteza rangi. Jambo hili ni dhahiri kuwa wahusika hawa waliishi katika hali ya umaskini na kupata mavazi mazuri ilikuwa shida.

Matukio ya mji wa Soweto yamedhihirisha kuwa walioishi katika mji huu walikuwa wa tabaka la maskini. Walioishi Soweto walikosa mavazi mazuri, waliishi katika vibanda, walifanya kazi ambazo zinamishahara midogo na walijihusisha na biashara ambazo hazina mapato.

Zaidi ya hayo, mwandishi ametumia mandhari ya mjini kuonyesha maisha ya tabaka la matajiri. Mwandishi anaelezea kuwa wenye mali wanakutana kwenye hoteli za kifahari kama vile Five Star Hotel International. Kupitia mhusika Farida tunapata mazungumzo ya watu waliokuwa hotelini wakizungumzia maisha ya matajiri. Farida anapomngoja Bwana Awori katika hoteli ili ampe kandarasi, Farida anapata fursa ya kusikiliza mazungumzo ya watu wawili waliokuwa karibu naye. Katika mazungumzo hayo walizungumzia jinsi matajiri wanamiliki mali. Matajiri hao wana magari ya kifahari, nyumba za kukodisha na pia wanaishi katika mitaa ya kifahari kama Runda jijini Nairobi. Pia mwandishi anatudokezea kuwa watoto wao wanaolewa nchi za ughaibuni kama Marekani.

Maisha katika miji ya kifahari ni tofauti na miji ya mabanda. Mwandishi anadhihirissha kuwa wanaoishi katika miji ya kifahari wanafanya mikutano katika hoteli za kifahari, kazi wanazofanya zina mshahara mkubwa. Mfano (uk. 178) Farida anapewa kandarasi na Bwana Awori ambayo ina mapato mazuri. Zaidi ya hayo wana nyumba za kukodisha. Wanaoishi katika miji ya mabanda kama Soweto wanapitia hali ngumu ya maisha. Vyumba vyao vinapatikana katika mazingira machafu. Mavazi wanayoyafaa yameraruka, hawana chakula cha kutosha na kupata pesa za kulipia kodi ya nyumba ni shida. Kupitia mandhari hayo mwandishi amefanikiwa kuwasilisha ujumbe wa utabaka.

Mandhari ya nyumbani yametumika kuwasilisha ujumbe wa utabaka. Mwandishi anatumia mandhari ya nyumbani kwa mzee Omar kuonyesha hali ngumu ya maisha waliyoyapitia. Kwanza tunachorewa karai iliyotumika na Kibibi mkewe Bwana Omar jinsi ilivyokuwa. Baada ya mzee Omar kuzidiwa na ugonjwa usiku, Kibibi anakimbia jikoni na kuleta maji baridi ya kumzindua Omar yakiwa yametiwa kwenye karai iliyokuwa inavuja. Hii ni ishara kuwa familia hii haikuwa na uwezo wa kununua karai nzuri na pia kupata pesa za kwenda hospitali kupata matibabu bora.

Zaidi ya hayo, chumba ambacho wanawe Omar, akina Farida, walilala kiliashiria watu wa tabaka la chini. Akina Farida walilala katika chumba cha kupumzika. Pia walilazwa katika jamvi kuukuu lililoongezwa magunia yaliyozeeka. Mambo haya yanadhihirisha kuwa familia hii haina uwezo wa kujenga nyumba ya vyumba vya kutosha vya kulala, na hawana pesa za kununua matandiko mazuri ya kulalia.

Tabaka la chini pia linadhihirika nyumbani kwa Mama Josii. Kupitia mhusika Kasu tunapata picha halisi ya nyumbani kwa Mama Josii. Kasu anapokaribishwa nyumbani kwa

Mama Josii anashuhudia mengi yanayomfanya kuhisi kuwa Mama Josii alipitia hali ngumu ya maisha. Watoto wa Mama Josii walilala sakafuni ambapo palitiwa jivu. Pia watoto hao walitandikiwa karatasi ambazo walizitumia kama godoro. Chumbani mwao mlikuwa na meza moja ambayo ililemaa na ilitingika kila wakati. Mandhari haya ya nyumbani kwa Mama Josii ni dhihirisho kuwa familia hii ilikuwa ya tabaka la chini.

Mwandishi ametumia mandhari ya nyumbani kwa mhusika Papi kuonyesha picha halisi ya mtu aliye na mali. Farida baada ya kujivinjari kwa vileo pamoja na Kim na Papi, Farida anaandamana na Papi hadi nyumbani mwake. Nyumba ya mhusika Papi ilikuwa kubwa na ya kifahari; ndani kulikuwa na vitu vya bei ghali kama, zulia jekundu, viti vya bei ghali na stima iliyoning'inia kila upande. Pia kulikuwa na kabati refu lililovutia jinsi lilivyorembeshwa. Zaidi ya hayo, katika mandhari haya tunatambua kuwa Papi alimiliki gari la kifahari aina ya Mercedes Benz. Kuwa na magari ya kifahari na nyumba illiyokuwa na samani ya bei ghali ni ishara kuwa alikuwa wa tabaka la matajiri.

Nyumbani kwa Mzungu ni kiwakilishi cha watu wa tabaka la juu (uk. 83). Mandhari hayo yanaonyesha mtu aliyemiliki mali. Mwandishi ametuchorea jinsi nyumba ya mzungu ilivyojengwa. Nyumba hii ilijengwa kwa kutumia mawe na kupakwa rangi ya manjano ukutani. Paa la nyumba hii ilikuwa ya muundo wa paa za Ulaya. Madirisha yalikuwa makubwa na yalitiwa vitambaa vya bei ghali. Mwandishi anazidi kueleza kuwa vyuma vilivyotumika kujengea nyumba hii viliagizwa kutoka nchi za ng'ambo. Nyumba hii pia ilizungukwa na ua wa umeme. Bwana White alikuwa amewaajiri wafanyakazi mbalimbali kama mlinzi na kijakazi. Ni katika mandhari haya ya nyumbani kwa Bwana White tunabaini kuwa Bwana White alimiliki bunduki. Kitendo cha kumiliki bunduki ni ishara kuwa Bwana White alikuwa tajiri na alihitaji bunduki kwa sababu ya ulinzi wake pamoja

na mali yake. “una bastola? Chini ya mto, mzungu alijibu.” (uk. 85) Zaidi ya hayo, mwandishi ametudokezea kuwa Bwana White alikuwa na pesa laki sita nyumbani kwake. Mambo haya yanadhihirisha kuwa Bwana White alikuwa wa tabaka la juu na mwandishi alitumia mandhari haya kudhihirisha tofauti ya tabaka la matajiri na maskini.

Mwandishi ametumia mandhari ya nyumbani kwa wahusika mbalimbali kudhihirisha ujumbe wa utabaka. Mandhari haya ya nyumbani yametoa picha halisi ya watu wa tabaka la matajiri na tabaka la maskini. Walio katika tabaka la chini mwandishi amedhihirisha kuwa walipitia changamoto nyingi za maisha. kupata pesa za matibabu ni shida, chakula kwao kilikuwa tabu na watoto wao walilala sakafuni. Walio katika tabaka la matajiri kama Bwana White walimiliki mali na kuishi maisha ya starehe. Bila mandhari hayo ingekuwa vigumu kwa mwandishi kufanikisha ujumbe wa utabaka.

#### 4.3.2. 2 Ujumbe wa Dhuluma

Dhuluma ni kitendo cha kumnyanyasa mtu kwa kumnyima haki zake, kumdunisha pamoja na kumtendea ukatili. *Kamusi Elezi* (2016:104), inaelezea dhuluma kama unyanyasi unaofanywa dhidi ya mtu mwingine, aghalabu kumnyima haki yake ya kimsingi. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), inaelezea dhuluma kama matendo ambayo hayana haki.

Ujumbe huu wa dhuluma umefanikishwa kupitia mandhari mbalimbali katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Mwandishi ametumia mandhari tofauti kutoa picha halisi ya vitendo vya dhuluma vinavyodhihirika katika jamii yake. Kwanza mandhari ya nyumbani kwa mhusika Papi. Mwandishi ametumia mandhari haya kuonyesha ukatili uliotendewa mhusika Farida. Baada ya Papi na Farida kulewa na kufika nyumbani kwa Papi usiku wa manane. Wanapofika nyumbani, Papi anafungua kabati kubwa, ndani lilikuwa na maiti ya msichana aliyerembeshwa. Papi anamtendea ukatili Farida kwa kumlazimisha kuosha

maiti ya msichana aliyekuwa kwenye kabati. Papi alitoa upanga wake aina ya Swodi na kumwelekezea Farida na kutoa amri ya kumpaka msichana huyo mafuta akiwa anatabasamu. Mwandishi anatudokezea kuwa Farida aliisugua maiti hiyo hadi ikawa laini. "Papi alifuta upanga wake wa aina ya swodi na akamuelezea kuwa chukukua mafuta na pamba na kumpaka msichana amwonaye katika kabati" (uk.22). Wakati huu ulevi aliokuwa nao Farida ulimwondoka. Mawazo mbalimbali yalianza kumrudia akiipaka mafuta maiti hiyo ila mawazo haya hayakumzuia kutofanya kazi aliyopewa. Upanga alioutoa Papi ulimfanya Farida kutekeleza yale aliyopewa. Mwandishi ametumia mandhari haya ya nyumbani kwa mhusika Papi kuonyesha jinsi Farida alivyodhulumiwa. Jambo hili lilikuwa la dhuluma kwa kuwa Farida alilazimishwa kuosha maiti bila ya yeye kukubali. Pia baada ya kuosha maiti, Farida anatishiwa na Papi kuwa akithubutu kusema kile alichokiona au kumweleza mtu yeyote yule, huo ungekuwa mwisho wake.

Katika mandhari ya hospitali ujumbe wa dhuluma unajitokeza. Mwandishi ametumia mandhari ya hospitali kuonyesha mateso ambayo wagonjwa wanapitia. Mandhari hayo ya hospitali yametoa picha halisi ya yale mambo ambayo wagonjwa wanapitia kwa sababu ya utepetevu wa manesi hospitalini na pia wasimamizi wa hospitali. Wasimamizi wa hospitali wanawadhulumu wagonjwa kwa kutowajibika katika kazi zao. Sakafu ilikuwa chafu kwa kukosa kupigwa deki kwa siku kadhaa. Jambo hili linadhihirisha kuwa wasimamizi wa hospitali hawatekelezi majukumu yao jinsi inavyostahili. Mandhari ya hospitali yanastahili kuwa safi. Manesi nao wanawanyima haki wagonjwa kupitia njia zifuatazo. Kwanza wanachelewa kufika kazini. Mwandishi anaonyesha jinsi ubao uliotumika kama kiti hospitalini ulikuwa umejaa. Wagonjwa walifika mapema hospitalini ili wapate matibabu ila wanapata kuwa daktari alikuwa hajafika.  Pia utepetevu wa madaktari unadhihirika pale

ambapo mgonjwa aliyefika kwa ajili ya kupata matibabu anafariki (uk. 35). Daktari alipofika hospitalini anasema kuwa ataanza na wale waliofika mapema. Hakujali kushughulikia mwanamke aliyezidiwa. Jambo hili linasababisha mgonjwa kufariki. Mandhari haya ya hospitali yamesaidia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wa udhalimu unaoendelea hospitalini na yametoa hali halisi ambayo wagonjwa walipitia katika jamii ya mwandishi.

Mandhari ya nyumbani kwa Bwana Marufuku yanafichua ujumbe wa dhuluma. Bwana Marufuku anadhulumiwa na mkewe baada ya kuwakaribisha watoto wa kaka yake marehemu Bwana Omar. Watoto hao walikuwa Farida na Kasu. Baada ya wazazi wa Farida na Kasu kufariki, Bwana Marufuku aliamua kuwachukua na kuwapeleka nyumbani kwake. Jambo hili halikupokelewa vyema na mkewe Marufuku. Bi Marufuku aliona bwana yake kama mtu mwenye mzaha kwa kuwachukua Farida na Kasu ilhali ameshindwa na kuwalea watoto wake kwa kilimo cha mihogo. Bi Marufuku alianza kumdhalilisha mume wakekwa kumtusi na kumwambia kuwa hana uume wa kufikiria yaani hafikiri kuhusu maswala ya familia yake. Mwandishi ametumia mandhari haya kuwasilisha mgogoro uliozuka baina ya Marufuku na mkewe. Ugomvi huu unasababisha Bwana Marufuku kunyimwa haki yake ya tendo la ndoa na mkewe. Jambo hili linasababisha Bwana Marufuku kuingiwa na unyama hadi kumnajisi mpwa wake Kasu. Mandhari hayo ya nyumbani yanatoa picha jinsi Bwana Marufuku alimdanganya Kasu hadi akamnajisi. Marufuku alimfanyia Kasu ujanja “njoo niende nikununulie nguo, na huko akamnajisi” (uk. 44).

Mwandishi pia ametumia Mandhari ya kazini kupitisha ujumbe wa dhuluma. Kupitia mhusika Juliet tunatambua kuwa alidhulumiwa na mwajiri wake. Mwandishi ametumia mandhari haya kuonyesha dhuluma ambazo Juliet alipitia akiwa kazini. Bwana Zarikha

ambaye ndiye alimwajiri Juliet, alikuwa anapitia jikoni na kuushika mwili wa Juliet bila ruhusa yake. Bwana Zarikha alikuwa anangojea mkwewe akitoka anampapasa Juliet. Jambo hili linasababisha Juliet kuamua kuacha kazi. Mandhari haya ya kazini yanafichua dhuluma za mapenzi wanazozipitia wafanyakazi wa nyumbani. Bila mandhari haya ya kazini ujumbe huu wa dhuluma haungewasilishwa vyema.

Mandhari ya nyumbani kwa mhusika Papi, Mandhari ya Hospitalini, mandhari ya nyumbani kwa Marufuku na mandhari ya kazini yamechangia katika kufanikisha ujumbe wa dhuluma katika jamii ya mwandishi. Mandhari haya yametoa picha halisi za dhuluma zinazoendelea katika jamii ya mwandishi. Kwa hivyo, mandhari hayo yamesaidia kufanikisha ujumbe wa mwandishi.

#### 4.3.2.3 Kudumisha Utamaduni

Wamitila (2003:33), anaeleza utamaduni kama uzoefu wa kimaisha wa watu fulani ambao huifanya jamii hiyo ijitambulishe na kujieleza. *Kamusi Elezi* (2016), inaeleza utamaduni kama desturi na mila za jamii. *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2004), inaeleza utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Kwa hivyo, utamaduni ni desturi na mila fulani zinazofuatwa na jamii.

Katika jamii ya *Maisha Kitendawili*, kuna tamaduni mbalimbali ambazo zinadhihirika kupitia mandhari tofauti. Kwanza mandhari ya mji wa Soweto. Mwandishi ametumia mandhari ya mjini kuwasilisha ujumbe wa utamaduni. Kupitia mhusika Kasu tunapata kundi la watu linalopatikana mjini Soweto. Kasu anashuhudia kundi hili likifanya utamaduni wao. Mhusika Kasu anapouliza kundi hilo linahusu nani anaambiwa ni kundi la Wagisu. Mwandishi anaeleza kuwa Soweto kuna watu wa asili tofauti. Kila kundi linafanya mambo yao kulingana na mila zao. Kwa hivyo, kundi hilo la Wagisu lilikuwa linatayarisha

wanaume kwa tohara. Kundi hili lilionyesha utamaduni wao kwa kucheza ngoma, manyanga na kayamba. Pia mikononi walikuwa na fimbo na vijana waliokuwa wanatayarishwa kupashwa tohara walikuwa uchi na walipigwa kwa matawi huku walioandamana nao wakiitikia kwa sauti. Mandhari haya yanatambulisha utamaduni wa jamii ya mwandishi na pia tunafahamu kuwa vijana wa siku hizi hawaelewi utamaduni. Mhusika Kasu huenda anaishi mandhari ambayo hayazingatii utamaduni kama wa kundi la Wagisu (uk.30).

Mandhari ya mazishini ya Bwana Omar na Kibibi pia yanaendeleza ujumbe wa utamaduni. Ni kupitia mandhari haya ambapo tunaelewa si kawaida watu kuzungumza katika mazishi. Ilikuwa kinyume na mila na desturi za jamii hiyo kuzungumza kwenye mazishi. Baada ya mazishi ya wazazi wa Farida kukamilika Chifu wa Lokesheni ya Mwasoko anapewa fursa ya kuzungumza na waombolezaji. Mwandishi anatudokezea kuwa ilikuwa si kawaida ya watu wenye cheo kama chifu kuzungumza kwenye mazishi. Wanajamii walidai kuwa kuzugumza ni kuhitilafiana na utaratibu wa kiitikadi. Mandhari ya mazishini yana mchango mkubwa kwa mwandishi kwa kuwa ameweza kueleza mila na tamaduni ambazo wanajamii walifuata wakati wa mazishi. Bila mandhari haya ingekuwa vigumu kutambua mila ambazo zinafuatwa wakati wa maziko.

Utamaduni pia unajitokeza kupitia mandhari ya nyumbani. Mandhari haya yamechangia katika kutambua utamaduni wa kuwa shughuli za nyumbani, pakubwa hufanywa na jinsia ya kike. Jambo hili limedhihirika kupitia nyumbani kwa Rose na nyumbani kwa Kasu. Nyumbani kwa Rose, Farida ndiye aliyeshughulika na kazi zote za nyumbani; mapishi, ufuaji nguo, upigaji deki wa sakafu na ununuzi wa vitu vidogo vidogo ndiye aliyefanya. Mwandishi ametumia mhusika Rose kudhihirisha kuwa Farida alikuwampishi hodari. Rose

anapokunywa chai kwa chapati ambacho kilipikwa na Farida anasema kuwa Farida alikuwa mpishi hodari.

Katika mandhari hayo ya nyumbani mwandishi anatumia mhusika Kasu kuonyesha akiyatekeleza majukumu ya nyumbani. Farida anapomtembelea dadake Kasu nyumbani kwake anampata akijishughulisha na kazi za upishi. Mjomba mumewe Kasu alikuwa amekaa sebuleni akipumzika. Kasu anapika ugali na pia nyama ambayo alitia nazi. Baada ya kupika Kasu anampakulia chakula Farida (uk. 145).

Utamaduni huu wa kuwa mwanamke ni mtumishi wa nyumbani, unafuatwa na jamii ya mwandishi. Hili limedhihirika kupitia wahusika Farida, Kasu na Mama Juliet ambaye alifanya kazi za nyumbani kwa Mhindi na baadaye nyumbani kwa Farida. Mwandishi ametumia mandhari ya nyumbani ili kudhihirisha utamaduni wa kuwa mwanamke ni mtumishi wa nyumbani.

Mwandishi pia ametumia mandhari ya nyumbani kwa Farida kuwasilisha utamaduni wa ndoa wa kufuata mila zilizowekwa na jamii kuhusu ndoa. Kupitia mhusika Juma tunampata anapendekeza kumuoa Farida. Mazungumzo haya ya ndoa yanaendelezwa nyumbani kwa Farida. Juma anapotaka kumuoa Farida bila kupitia utaratibu wa utamaduni wa kuifahamisha jamaa yake kuhusu ndoa hiyo. Farida anamwonya vikali kuhusu jambo hili. Mhusika Farida anamwelezea Juma kuwa lazima haifahamishe jamaa yake kabla ya kumpa jibu la kuoana. Farida ni mhusika aliyelelewa katika mandhari ya mashambani kabla ya kuhamia mjini. Ingawa Farida amekengeuka pakubwa baada ya kuhamia mjini, jambo hili la utamaduni wa ndoa analitia maanani. Ndiposa anamshauri Juma kwamba ingestahili

kwanza ampe muda ili azungumze na jamaa yake kuhusu swala la ndoa. Kwa hivyo, mandhari haya ya nyumbani ni muhimu katika kufanikisha ujumbe wa utamaduni wa jamii.

#### 4.3.2.4 Uvumilivu katika Ndoa

Ndoa ni taasisi muhimu katika jamii. Imani za kidini, mila na desturi na hata sheria za nchi huthamini sana taasisi ya ndoa. Ndoa katika Ukristo huchukuliwa kama mahusiano yaliyoidhinishwa na Mungu mwenyewe. Uhusiamo huu unatakiwa kudumu katika maisha yote ya wahusika wanaooana. Biblia huwa inawaidhinisha wale wanaooana kuwa mwili mmoja baada kuunganishwa katika harusi. Mke na mume huwa mwili mmoja na damu moja (Biblia, Mwanzo 1:21-24).

Biblia inazidi kudokeza katika Waefeso (5:22-28) kuwa wake wanapaswa kuwatii waume zao kwa kuwa kufanya hivyo ni kama kumtii bwana Kristo. Mume amechukuliwa kama kichwa cha mke, hivyo anastahili kumtii mume kwa kila jambo. Pia wanaume naowanastahili kuwapenda wake zao kama Kristo alivyolipenda kanisa na akajitoa kwa ajili yake. Muungano huu wa ndoa katika Biblia unadokeza kuwa muungano huu haustahili kuvunjika hadi siku ya kifo. Mungu huwapa neema zinazohitajika waweze kutimiza malengo yao ya ndoa.

Dini ya Kiislamu ina mtazamo wao kuhusu ndoa. Kulingana nao ndoa ni mapatano ya kisheria kati ya mwanamke na mwanamume. Mapatano haya hufanywa kwa njia ya mkataba ambao wakati mwingine huwa kupitia njia ya maandishi na hushuhudiwa na mashahidi wawili pamoja na mlezi wa bibi arusi. Vilevile dini ya Kislamu hutilia mkazo swala hili la ndoa kupitia tamko la Mtume Muhammad likiaminika linatoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammad alisema kuwa ndoa ni ya yule anao uwezo wa kuoa na aoe kwa kufanya hivyo, kutamsaidia kuepukana na usherati (Quran 4:25). Katika ndoa ya

Kiislamu, mwanamume anaruhusiwa kuoa jumla ya wake wanne. Jambo hili linaruhusiwa iwapo mwanamume ana uwezo wa kuwatunza na kuwapenda wake wote kwa usawa. Kuoa wake wengi kulisaidia kupunguza mambo ya uasherati (Quran, 4:3).

Katika utamaduni wa jadi, ndoa ilichukuliwa kama muungano wa mume na mke katika kuanzisha familia yao. Ndoa ndiyo huendeleza vizazi vijavyo katika jamii. Jamii hupanuka na kukuzwa kupitia asasi ya ndoa. Mbiti (2014), anaeleza kuwa utamaduni wa jadi wa ndoa huchukuliwa kuwa ndoa imekamilika inapokuwa na watoto na hasa wa kiume. Mtoto wa kiume alichukuliwa kama nguzo ya jamii. Tamaduni nyingi za Kiafrika, mwanamke akiolewa watoto wake huwa sehemu ya ukoo wa mumewe. Ndoa za kitamaduni sharti kuwepo na idhini ya wazazi, la sivyo ndoa hiyo haitatambuliwa.

Malengo makuu ya ndoa iwe ya kitamaduni, Kikristo au Kiislamu ni mume na mke kuishi kwa upendo, kufurahishana kwa njia ya tendo la mapenzi, kuzaa na kulea watoto na kuvumilia katika ndoa.

Katika jamii ya *Maisha Kitendawili*, mwandishi amewasilisha ujumbe wa uvumilivu katika ndoa kupitia mandhari mbalimbali. Kwanza mandhari ya nyumbani kwa Bwana Omar na mkewe Kibibi (uk.32-34). Ndoa hii inakumbwa na changamoto nyingi ila wahusika hao walionyesha uvumilivu katika ndoa yao. Katika nyumba ya Bwana Omar mwandishi anatumia mandhari hayo kuonyesha changamoto walizopitia wanandoa hawa wawili licha ya ndoa yao kuwa thabiti. Mwandishi anatuonyesha vile mhusika mzee Omar alivyopitia hali ngumu ya maisha kwa sababau ya ugonjwa wa pumu. Mzee Omar alizaliwa akiwa na matatizo ya mapafu. Kila mmoja katika nyumba hii alikuwa amezoea hali ya mzee Omar

ya taabu hasa wakati wa mvua na kipupwe. Mkewe mzee Omar alijifunza kuvumilia hali hii na kumtunza mumewe.

Mwandishi anatoa picha halisi ya shida wanazopitia wahusika hao wakiwa nyumbani. Bwana Omar anapozidiwa na ugonjwa, Kibibi kwa moyo wa imara na kijasiri anamhudumia mumewe kwa kumpa huduma ya kwanza. Kibibi anamlaza Bwana Omar na kumpangusa povu iliyomtoka kwa kutumia shuka. Pia alikimbia jikoni na kuleta maji baridi ya kumzindua mumewe. Licha ya umaskini uliowakumba Kibibi alijikakamua ili kumsaidia mumewe.

Mandhari haya yanaonyesha familia iliyopitia changamoto nyingi sana. Kwanza Kibibi anatumia ncha ya shuka kumpangusa mumewe iliyotumika kama blanketi (uk. 33). Pia karai aliyoitia maji Kibibi ilikuwa inavuja. Baada ya Omar kuzidiwa na ugonjwa, Kibibi anamlaza katika chumba cha kupumzika. Katika chumba hiki ndiko wanawe Omar walilala. Jamvi kuukuu lililotumiwa kama matandiko ya wanawe. Matandikio haya yalikuwa yametandikwa magunia na maleso yaliyozeeka. Licha ya kuolewa katika mandhari ya taabu, Kibibi anavumilia katika ndoa yake na kutekeleza majukumu ya kumtunza bwanake na watoto wake.

Mandhari ya nyumbani kwa Bwana Marufuku yanafichua ujumbe wa ndoa iliyokuwa inakumbwa na misukosuko na usaliti wa ndoa. Mwandishi anatumia mandhari haya kuonyesha ndoa iliyokuwa na usaliti ila wanandoa hawa wanazidi kuishi pamoja. Marufuku alikuwa mjomba wa Kasu na Farida, ndiye aliyewachukua na kuishi nao baada ya wazazi wao kufariki. Ukaribisho huu wa Farida na Kasu unazua ugomvi baina ya Marufuku na mkewe. Bi Marufuku anatofautiana na mumewe kuhusu jambo hili la

ukaribisho wa Farida hadi mkewe Marufuku anaanza kumdharau mumewe. Ndoa za kitamaduni, Kikristo au Kiislamu zote zilimthamini mwanamume kama kiongozi wa nyumba na ambaye anastahili kuheshimiwa. Bi Marufuku alivunja utamaduni huo na kumdhalilisha mumewe licha ya mumewe kuomba msamaha. Jambo hili linasababisha bwana Marufuku kunyimwa tendo la ndoa na mkewe, anamnajisi mpwa wake Kasu. Licha ya tofauti hizi na changamoto walizopitia wanandoa hao, walivumiliana na kuishi kama familia moja (uk. 44).

Mwandishi pia ametumia mandhari ya nyumbani kwa Mama Josii kuendeleza ujumbe wa uvumilivu katika ndoa. Mama Josii anaonyesha uvumilivu na mapenzi ya dhati kwa familia yake licha ya mumewe kuwa mgonjwa. Majukumu yote ya nyumbani yaliachiwa Mama Josii. Mama Josii ndiye aliyetafuta pesa kulipia gharama ya matibabu, chakula na pia ndiye aliyegharamia elimu ya watoto wake. Familia hii ilipitia changamoto nyingi kama, nyumba yao ilivuja maji paani na ukutani, kupata chakula cha kutosha katika nyumba hiyo ilikuwa jambo gumu. Licha ya hayo Mama Josii anavumilia na kugharamia mahitaji ya familia (uk. 68). Kwa hivyo, mandhari ya nyumbani kwa Bwana Omar, kwa Marufuku na kwa Mama Josii yamechangia kufanikisha ujumbe wa uvumilivu wa ndoa. Wahusika hawa walipitia changamoto nyingi katika ndoa zao ila wanavumilia.

### 4.4.0 Ujumbe katika riwaya ya Rosa Mistika

#### 4.4.1 Utangulizi

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* ameangazia mambo ambayo hutokea katika Jamii yake. Baadhi ya mambo hayo ni uvumilivu wa ndoa, utabaka unaodhihirika katika jamii, nafasi ya mwanamke, dhuluma wanazopitia wanajamii na utamaduni unaozingatiwa katika jamii ya mwandishi. Ujumbe huu wa mwandishi umedhihirika kupitia mandhari

mbalimbali kama mandhari ya shuleni, mandhari ya nyumbani, mandhari ya baa na mandhari ya chuoni.

### 4.4.2 Uvumilivu katika Ndoa

Katika jamii ya mwandishi wa*Rosa Mistika*, mwandishi amepitisha ujumbe wa uvumilivu katika ndoa kupitia mandhari mbalimbali. Kwanza mandhari ya nyumbani kwa mhusika Regina. Mbiti (2014) anaeleza katika utamaduni wa jadi, ndoa ilichukuliwa kuwa imekamilika inapokuwa na watoto na hasa wa kiume. Hii ni kwa sababu mtoto wa kiume aliaminiwa kuwa nguzo ya jamaa. Kupitia mandhari haya ya nyumbani kwa Bi. Regina mwandishi amesawiri ndoa iliyokumbwa na shida nyingi. Mwandishi anatudokezea kuwa katika kijiji cha Namangondo ambapo Regina aliishi alipigwa karibu kila juma. Alikuwa anateswa na kusumbuliwa na mumewe kwa kosa lisilo lake. Bi Regina alipopata ujauzito alikuwa anautuza vizuri. Alikuwa habebi vitu vizito na alikuwa halali kifudifudi akiogopa kuharibu mimba. Licha ya kutunza mimba hakufanikiwa kupata mtoto wa kiume. Bwana Zakaria aliendelea kumpiga mke wake na kumdhalilisha kwa kupata watoto wa kike pekee. Mhusika Regina licha ya kuteswa na mumewe alivumilia katika ndoa yao. Pia alionyesha mapenzi kwa watoto wake pamoja na mume wake Zakaria ambaye alikuwa mlevi kupindukia.

Katika mandhari ya nyumbani kwa mwalimu mkuu wa Chuo cha Ualimu tunapata ujumbe wa usherati na usaliti katika ndoa. Mwandishi ametumia mhusika Rosa kuonyesha jinsi alivyovuruga ndoa za watu. Rosa anamtembelea Bwana Thomas katika nyumba yake ambayo ilikuwa katika mandhari ya chuoni. Nyumbani, Rosa alikaribishwa kwa kinywaji cha pombe. Katika hali hii ya kubugia pombe mapenzi ya Rosa na Bwana Thomas

yalipamba moto. Mwalimu Thomas aliamua kumdhalilisha mke wake. Baada ya Rosa kulewa anafanya mapenzi na mwalimu Thomas.

Ndoa hiyo inadhihirisha uvumilivu. Hii ni kwa sababu mwalimu huyu ana mke wake wa halali na anajiingiza katika uasherati na ukosefu wa uadilifu. Hatimaye Bwana Thomas na Rosa wanafumaniwa na mke wa mwalimu mkuu (uk. 54). Mwandishi alieleza kuwa mke halali wa mwalimu mkuu alikuwa tayari amewafumania kwa kuwa alikuwa anawasikiliza dirishani. Maneno aliyoyasikia yalifanya kupandwa na hasira na kuamua kupasua mlango kwa shoka. Kitendo hiki cha kupasua mlango kinadhihirisha huyo ndiye mke halali wa Bwana Thomas. Zaidi ya hayo, kupitia kwa mke wa mwalimu mkuu tunatambua kuwa si mara ya kwanza yeye kumfumania mumewe akifanya usaliti. Kitendo hiki cha usaliti kinafanya Rosa kupata maumivu kwenye mwili wake na baadaye kufukuzwa chuoni. Mwandishi ametumia mandhari hayo ya nyumbani kuwasilisha ujumbe wa uvumilivu wa ndoa katika jamii ya mwandishi.  Licha ya usaliti huu mke wa mwalimu mkuu anavumilia na kusalia katika ndoa.

Ndoa nyingine inayodhihirisha uvumilivu ni ndoa ya Ndalo na mkewe Bigeyo. Mandhari ya nyumbani kwa Bwana Ndalo na mandhari ya mazishini yanaendeleza ujumbe wa uvumilivu katika ndoa. Mhusika Regina alipowatembelea Ndalo na mkewe Bigeyo nyumbani kwao ili kujua kuhusu kile kilichofanya Zakaria kulewa zaidi. Regina anawapata Ndalo na mkewe Bigeyo wanakula nyama ya kuku huku wanakimbia kuzunguuka nyumba yao. Jambo hili linadhihirisha kuwa familia hii ilisumbuliwa na jambo fulani. Familia hii ilikosa kubarikiwa na mtoto. Ndalo pamoja na mkewe Bigeyo wamepitia hali ngumu wakitafuta mtoto. Wamepoteza pesa nyingi wakitafuta dawa ya uzazi. Pia wametafuta usaidizi kwa waganga na pia hospitalini hadi madaktari wakawaarifu hawatapata mtoto.

Itikadi zilizopitwa na wakati zilisababisha familia hii kulaghaiwa kwa ajili ya kutafuta mtoto.

Familia hiyo iliishi pamoja hadi kifo cha Bwana Ndalo. Bwana Ndalo hakuvunja ndoa yake alivumilia na kustahimili shida za mke wake na kuishi kama mke na mume. Kifo cha Bwana Ndalo kilihuzunisha Bigeyo. Hili linadhihirika katika siku ya mazishi. Bi Bigeyo alilia kwa sauti na kuuliza mumewe kwa nini amemuacha. Bi. Bigeyo alitamani wangefariki pamoja kwani walistahimili shida pamoja. Mwandishi alitumia mandhari haya kudhihirisha kuwa familia zinaweza kuishi kwa upendo na uvumilivu licha ya kukosa kubarikiwa kupata watoto.

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika*ametumia mandhari ya nyumbani, chuoni na mazishini kuonyesha ujumbe wa uvumilivu wa ndoa. Mandhari hayo yametoa picha halisi ya mambo waliyopitia wanandoa hao na kuvumilia katika ndoa zao.

### 4.4.3 Nafasi ya Mwanamke katika jamii

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* amechora mwanamke katika mitazamo mbalimbali. Mitazamo hii imedhihirika kupitia mandhari tofauti tofauti. Kwanza mwanamke amechukuliwa kama mlezi bora katika jamii. Mlezi ni hali ya kuwaongoza watu wa familia kuishi katika mielekeo mbalimbali ya maisha. Mielekeo hiyo inaweza kuwa bora au isiyo bora. Ulezi ni kazi ambayo inahitaji juhudi za kila mmoja katika familia. Ushirikiano mzuri baina ya mume na mke huimarisha malezi ya watoto. Jukumu la ulezi katika riwaya ya *Rosa Mistika* limeachiwa wanawake. Ujumbe huu wa mwanamke kama mlezi bora unadhihirika kupitia mandhari ya nyumbani.

Mhusika Regina anatupa picha halisi ya mwanamke aliyejitolea katika ulezi wa wanawake. Katika mandhari ya nyumbani kwa Regina mwandishi anaonyesha jinsi Regina alichukua fursa ya kuwapa wosia watoto wake wakati wa jioni (uk. 11). Regina alitumia muda huu kuwaonya binti zake. Regina aliwaonya waepukane na tabia kama kuongea uwongo, wasiwe wavivu na pia kumpa baba yao heshima inayostahili licha ya kuwa mraibu wa pombe. Mawaidha aliyowapa yalitegemea umri wa watoto wake. Kwa kuwa mhusika Rosa alikuwa amebaleghe alimwonya kuepukana na wavulana wakorofi. Kwa hivyo, mandhari haya ya nyumbani yamechangia kuwasilisha ujumbe wa nafasi ya mwanamke katika jamii kama mlezi bora.

Mwanamke pia ameonyeshwa kama mzalishaji mali katika jamii. Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* ametumia mhusika Regina kama mzalishaji mali. Kupitia mandhari ya nyumbani kwa mhusika Regina tunapata ujumbe huu. Mandhari haya yanatusaidia kuelewa kuwa Regina alijishughulisha na kazi ya kilimo cha pamba, mihogo na ufugaji wa mifugo. Regina alilima pamba kwa bidii na pesa alizopata kutokana na ukulima huo ndizo alizotumia kuwalisha watoto wake pamoja na mume wake. Pia mifugo aliowafuga walimsaidia katika kuelimisha Rosa na Flora. Mandhari haya ya nyumbani kwa Regina yanadhihirisha jinsi Bi. Regina anajikakamua kutafuta pesa za kumpeleka Rosa shuleni, baada ya ng’ombe aliofuga kuuzwa na mumewe kwa ajili ya kunywa pombe. Regina anakata shauri kutayarisha pombe ya mihogo ili kupata karo ya shule (uk. 19). Regina alipika pombe mapipa matatu na kuuza akisaidiwa na binti zake. Baada ya mapipa hayo kuisha pombe walihesabu pesa ambazo walipata na kufurahi kwa kuwa zitawasaidia kumpeleka Rosa shuleni. Kwa hivyo, bila mandhari haya ingekuwa vigumu mwandishi kuonyesha kazi ambazo Regina alifanya na manufaa ya kazi hizo.

Mwanamke ameonyeshwa kama chombo cha starehe. Ujumbe huu umedhihirika kupitia mandhari ya shuleni na chuoni. Mwandishi ametumia mhusika wa kike Rosa kuonyesha jinsi alitumika kama chombo cha starehe akiwa shule ya Rosary. Rosa alibadili tabia alipofika kidato cha tatu baada ya kushawishiwa na rafiki yake Thereza. Mandhari haya ya shuleni yanadhihirisha vile Rosa alivyobadili tabia. Mwanzoni Rosa alikataa ushawishi wa picha za wavulana kutoka kwa Thereza ambaye alikuwa mwandani wake. Hatimaye, Rosa alibadili nia na akawa anaenda dansi na kuchezea wavulana jinsi alivyotaka. Ni katika mandhari haya Rosa anakutana na Bwana Deogratius ambaye wanakuwa wapenzi.

Mhusika Rosa anapojiunga na Chuo cha Ualimu cha Morogoro anaendelea kutumika na wanaume kama chombo cha starehe. Mwandishi anaonesha mhusika Rosa akibadilisha wavulana jinsi apendavyo ilimradi apate pesa. Katika mandhari haya ya chuoni tunatambua kuwa Rosa alipewa jina la utani "laboratory". Mhusika Rosa alitumiwa kama chombo cha majaribio, kwani mvulana yeyote aliweza kufanya jaribio lake la kukutana na Rosa kimwili. Mwandishi anathibitisha haya anapochora vijana chuoni wakisoma gazeti kuhusu njia za kufanya ngono. Wale ambao hawajatumia njia zilizoelezwa katika gazeti wanaelekezwa wajaribu kupitia mhusika Rosa.

Zaidi ya hayo, mwandishi anazidi kumchora mhusika Rosa kama anayetumika kama chombo cha starehe na Mwalimu Mkuu katika mandhari ya nyumbani kwa Bwana Thomas. Katika mandhari haya, Rosa anamtembelea Mkuu wa Chuo nyumbani kwake na kushiriki mapenzi naye. Jambo hili la kutembelea mkuu wa chuo linasababisha wao kufumaniwa na mkewe halali wa Bwana Thomas. Uasherati huo unasababisha Rosa kuumizwa kwa kupigwa na kukatwa sikio. Matukio haya ya shuleni yamedhihirisha jinsi mwanamke alivyotumika kama chombo cha starehe. Rosa shuleni alichezewa na wavulana, chuoni

alitumika kama chumba cha majaribio na nyumbani anafanya mapenzi na Bwana Thomas ambaye alikuwa ameoa.

### 4.4.4 Ujumbe wa Dhuluma

Dhuluma ni tendo la kumyanyasa mtu kwa kumnyima haki zake, kumdunisha pamoja na kumtendea ukatili. *Kamusi Elezi* (2016:104), inaeleza dhuluma kama unyanyasaji unaofanywa dhidi ya mtu mwingine aghalabu kumnyima haki yake ya msingi.

Ujumbe huu wa dhuluma umepitishwa kupitia mandhari mbalimbali katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Kwanza kupitia mandhari ya kijiji cha Namagondo. Katika kijiji hiki tunapata mhusika Regina ambaye aliolewa na Zakaria (uk. 3). Bwana Zakaria anamdhulumu mkewe Regina kwa kumpiga kila mara. Jambo ambalo Zakaria alidai lilimfanya kumpiga mkewe ni kuwa hakumzalia mtoto wa kiume. Wanawake wa kijiji hicho walimwonea huruma Regina kwa kuwa kudhulumiwa kwake hakumfanyi kutoka kwenye ndoa yake. Zaidi ya hayo, Bwana Zakaria alitoa vitisho kwa Regina na watoto wake. Vitisho hivi vilifanya Regina na watoto kuwa na woga. Jambo hili lilifanya watoto kukimbilia vitandani mwao na hata wakati mwingine walishauriwa na Bi. Regina kutorokea katika chumba cha kulala waliposikia sauti ya Bwana Zakaria. Pia wakati mwingine wanalazimika kulala mapema kwa kuhofia Bwana Zakaria. Bwana Zakaria anapofika nyumbani akiwa mlevi analazimisha Regina kuwaamsha watoto. Wanapoamka wanalazimishwa kuimba usiku. Kupigwa kwa Regina, kutoa vitisho kwa watoto na kuamshwa usiku, kuwalazimisha kuimba na pia Zakaria kuuza ng’ombe na kutumia katika ulevini vitendo vya dhulumu.

Ujumbe huo wa dhuluma pia unadhihirika nyumbani kwa Zakaria, pale ambapo mhusika Rosa anapigwa na baba yake Bwana Zakaria. Bwana Zakaria anampiga Rosa kwa kosa la kuandikiwa barua na Charles. Rosa anatendewa ukatili na babake kwa kupigwa makofi

mfufulizo hadi damu ikamtoka puani na mdomoni. Mhusika Rosa anapoomba msamaha, baba yake anazidi kumpiga na hata kumnyang'anya shuka na kuachwa akiwa uchi. Jambo hili linadhihirisha dhuluma kwa Rosa.

Mwandishi alitumia mandhari haya ya nyumbani kujenga taswira halisi ya ukatili na unyanyasaji uliofanyiwa Rosa. Kitendo hiki cha kupigwa kinamfanya Regina mamake Rosa kububujikwa na machozi na kulia kwa sauti ili kumwokoa binti yake. Zaidiya hayo, ukatili huu unazidi pale Bwana Zakaria anamkaba koo Rosa hadi macho ya Rosa yakawa mekundu.

Kubakwa ni tendo la kufanya ngono kwa kutumia nguvu (*Kamusi Elezi* 2016:33). Tendo hili la kubakwa ni dhuluma kwa jinsia ya kike. Kupitia mandhari ya nyumbani kwa mhusika Charles, tunapata kitendo cha ubakaji. Mhusika Charles anambaka Rosa baada ya wahusika hawa kulewa. Charles anamnajisi Rosa na kumlaza chini sakafuni na kumwosha ili Rosa asijue. Kitendo hiki kinadhihirisha ukatili uliofanyiwa mhusika Rosa kwa kubakwa. Bila mandhari haya ya nyumbani kwa Charles ingekuwa vigumu mwandishi kufanikisha ujumbe wa dhuluma kwa kuwa mandhari hayo yametoa picha halisi ya yale yaliyotokea.

Mandhari ya nyumbani kwa Bwana Zakaria yanafichua ujumbe wa dhuluma. Watoto wa Bwana Zakaria, ambao ni Flora, Stela, Honorata, Sperantia na Emmanuel wanadhulumiwa kwa kunyimwa haki yao ya urithi. Jamaa yao baada ya mazishi ya Zakaria, mkewe Regina na mwana wao Rosa walibaki nyumbani wakiomboleza. Wakati huu wa maombolezo, jamaa hawa walihakikisha kuwa wamewachinja ng'ombe wote walioachwa na Bi. Regina. Baada ya ng'ombe wa mwisho kuchinjwa, kuna wengine walioachwa ili kugawana urithi

wa Bwana Zakaria. Jamaa hawa waliamua kurithi kila kitu kilichoachwa na marehemu Zakaria. Kwanza walianza kwa kurithi chochote kilichokuwa ndani ya nyumba. Kisha pesa ambazo zilikuwa benki, mimea yote iliyokuwa kwenye shamba la Zakaria na pia mnyama yeyote aliyekuwa kwenye boma hilo. Mwandishi ametumia mandhari haya kufanikisha ujumbe wa dhuluma uliofanyiwa watoto wa Bwana Zakaria. Jamaa hawa hawakuwa na utu kwani walinyakua kila kitu kilichoachwa kama urithi.

Mwalimu Mkuu wa Chuo cha Ualimu, Bwana Thomas anamdhulumu mkewe kwa kumwingiza Rosa nyumbani kwake na kufanya mapenzi naye. Mandhari haya ya chuoni yanatudokezea jinsi Rosa alifanya mapenzi na Mwalimu Mkuu nyumbani kwake. Mwandishi anatuelezea kuwa humo chumbani Mkuu wa Chuo Bwana Thomas alimwomba Rosa avue nguo wakalale. Baada ya kuvua nguo walikaa kitandani ambacho ni kitanda cha mke halali. Kitendo hiki kinamdunisha mke wa mkuu wa Chuo. Jambo hili lilifanya wao kufumaniwa na mke wa Mkuu wa Chuo na Rosa kupigwa hadi akapata majeraha ya mwili.

Kwa hivyo bila mandhari ya kijiji cha Namagondo, mandhari ya nyumbani kwa Zakaria, nyumbani kwa Charles na mandhari chuoni ingekuwa vigumu mwandishi kufanikisha ujumbe wa dhuluma zinazotokea katika jamii yake.

### 4.4.5 Utamaduni

*Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2004), inaelezea utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Kwa hivyo, utamaduni ni desturi na mila fulani zinazofuatwa na jamii. Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, utamaduni wa jamiii ulidhihirishwa na mandhari mbalimbali. Kwanza mandhari ya mazishini. Katika mazishi ya Bwana Ndalo ujumbe wa utamaduni unajitokeza. Jamii hii ilifuata mila na taratibu zao wakati wa mazishi. Kwanza, watu wa jamii hii lazima wakati wa mazishi kuhudhuria mazishi. Hili linadhihirishwa na

wahusika kama Rosa na Charles wanaotoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kuhudhuria maziko. Pia wakati wa matanga wanajamii wanawatembelea wanaomboleza kwa ajili ya kuwaliwaza. Zaidi ya hayo, ilikuwa mila na desturi za jamii kaburi kuchimbwa, na maiti ilipaswa kuoshwa kabla ya kuzikwa. Familia ya marehemu ilistahili kukaa karibu na jeneza kabla ya maziko. Jambo hili linadhihirika kupitia mhusika Bigeyo mke wa marehemu Ndalo. Bigeyo alikaa karibu na maiti ya mumewe. Pia mwili wa marehemu Ndalo ulioshwa kabla ya maziko. Kwa hivyo, mandhari haya ya mazishi yanafanikisha ujumbe wa utamaduni ambao hufuatwa wakati wa mazishi katika jamii ya mwandishi.

Mandhari ya nyumbani kwa marehemu Zakaria, Regina na Rosa, yanafanikisha ujumbe wa utamaduni. Mwandishi anaeleza kuwa katika kijiji cha Namagondo baada ya kupata habari za kifo cha Zakaria, Regina na Rosa, wanajamii walimiminika nyumbani kwa marehemu kushuhudia yaliyotokea. Watoto katika kijiji hicho wanatambua kitu fulani kimetokea kwa utulivu unaokuwa wakati wa maombolezo. Isitoshe, katika kisiwa hiki cha Namagondo wanajamii wanaamini kuwa ndege anayejulikana kama bundi anaposikika maafa hutokea. Usiku watoto waliposikia mlio wa bundi walijikunja vitandani kwa kuhofu maafa zaidi.

Kutokana na mandhari haya tunaona kuwa jamii ya mwandishi ilifuata utamaduni wao. Mila na taratibu mbalimbali zilifuatwa wakati wa mazishi na pia ndege kama bundi waliaminika husababisha maafa katika jamii. “Usiku wa manane bundi walianza kusikika. Watoto walijikunja vitandani, watu wa kisiwa hiki waliamini kwamba bundi akilia karibu na mji kifo hutokea humo. Kwa hivyo bundi walipotoa sauti hofu ya watu iliongezeka” (uk. 93). Utamaduni huu ni halisi katika jamii ya mtafiti kwani ndege aina ya bundi aliaminika sana kuwa hakisikika sauti yake usiku maafa yatatendeka katika jamii hiyo.

Wanajamii walimfurusha kwa kutumia vigae vya chungu ili kujilinda kutokana na maafa hayo.

### 4.4.6 Utabaka

Asili ya utabaka ni mfumo wa uzalishaji mali kuanzia utumwa, umwinyi na ubepari. Jamii nayo ikagawanyika dhahiri na kuwa na matajiri na maskini. Matajiri wakawa na maeneo yao ya kifahari wanamoishi na maskini wakawa na maeneo yao ya mabanda. Jambo hili likazaa mandhari ya matajiri na mandhari ya maskini. Watu wa tabaka la juu (matajiri) wakawa ni wale wanaomiliki mali, wanaishi maisha ya starehe, nyumba zao ni za kifahari, wanamiliki magari ya kifahari, wanalindwa mchana na usiku, chakula kwao si shida na wanawadhulumu wasiokuwa na mali. Watu wa tabaka la chini (maskini) nao waliishi kwenye maskani duni, wanalipwa mishahara duni, wanakosa mavazi mazuri na hawana kazi ambazo zinatosheleza mahitaji ya nyumbani. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* jamii iligawika katika matabaka mawili. Tabaka la matajiri na tabaka la maskini. Matabaka haya yamedhihirika kupitia mandhari ya nyumbani na mjini.

Mwandishi amedhihirisha tabaka la maskini kwa kutumia mandhari ya nyumbani kwa mhusika Zakaria. Familia ya Bwana Zakaria iliishi kwenye maskani duni ambayo yalidhihirishwa na jinsi nyumba yao ilivyozeeka, ilivuja sana wakati wa mvua inavyonyesha (uk. 13). Pia watoto wa Zakaria walilalia matandiko ambayo yalizeeka na yalikuwa yameliwa na mchwa. Jambo hili linadhihirisha kuwa ilikuwa vigumu kupata malazi mazuri kwa kuwa mapato yao yalikuwa duni.

Kazi ambazo familia hii ilifanya ilikuwa kazi ya ukulima. Bi. Regina alifanya ukulima wa pamba na mihogo. Mapato waliyopata kutoka mazao ya mimea hii yalikuwa ya chini. Mfano Bi. Regina aliuza mihogo ili kupata karo ya binti yake Rosa ila hakufanikiwa kupata

pesa za kutosha. Jambo hili lilimlazimu kutayarisha pombe na kuuza. Kwa hivyo, mwandishi alitumia mandhari haya ya nyumbani kwa Zakaria kuonyesha shida ambazo familia hii ilipitia. Bila mandhari haya, ujumbe wa tabaka la chini haungedhihirika vizuri. Zaidi ya hayo, familia hii ya Zakari iliendelea kudhihirisha kuwa ilikuwa ya tabaka la chini. Jambo hili linatokea pale ambapo Bwana Zakaria anapokea barua ya kutembelewa na mgeni. Barua hii ilifanya Bwana Zakaria kuwaza ni wapi mgeni huyo atalala. Zakaria aliona aibu mgeni kulala katika nyumba yenye chumba kimoja. Hii ni ishara kuwa familia hii ilikuwa haina uwezo wa kujenga nyumba ya vyumba vya kutosha. Pia ingekuwa aibu mgeni wa heshima kama Bwana Deogratias kulala sebuleni ambapo watoto wa Zakaria walilala. Mandhari haya ya nyumbani kwa Zakaria yamechangia kupitisha ujumbe wa utabaka.

Mandhari ya mjini katika duka la Mhindi yanafanikisha ujumbe wa utabaka. Mwandishi anaonyesha jinsi duka la Mhindi lilikuwa na bidhaa za bei ghali. Jambo hili linajitokeza wakati wahusika Rosa na dadake Flora wanaenda kununua viatu vya Rosa kwa ajili ya kujiunga na shule.  Uamuzi wa Rosa kununua katika duka la Mhindi ni kuwa mjomba wake Ndalo ndipo alifanya kazi. Rosa walijaribu kuulizia bei ya viatu na kupata vilikuwa vya bei ghali. Walijaribu kumshawishi kupunguza bei ila mwenye duka alikataa. Ni katika mandhari haya tunapata mwenye duka anamnyanyasa Ndalo kwa kumfokea na kumtusi. Jambo hili linatokea baada ya mhusika Ndalo kuwaelekeza Rosa mahali wangepata viatu vile walivyokuwa wanataka kwa bei nafuu. Bwana Mhindi anamtupa nje Bwana Ndalo na kumtupia shilingi tano. Kupitia mandhari haya ya dukani tunapata dhuluma ambazo watu wa tabaka la chini wanapitia mikononi mwa matajiri.

Mkuu wa wilaya, Bwana Deogratias ni mmoja wa watu wa tabaka la juu. Mkuu huyu alikuwa kiongozi aliyemiliki mali. Kupitia mandhari ya kisiwani Mwanza, tunaona Bwana Deogratias aliwadhulumu vijana kwa kuwapachika mimba na kuwapa pesa kwa kuwa alikuwa nazo (uk. 41). Zaidi ya hayo, alitumia cheo chake kutenda maovu kisha anatumia cheo hicho, pamoja na pesa, kusingizia kuwa maovu hayo yalitendwa na wengine. Mwandishi anatudokezea kuwa Bwana Deogratias amekwisha watia mimba watoto wawili wa shule. Baada ya kutenda maovu hayo aliwapa pesa na wakataja vijana wengine waliokuwa wakisoma nao na kulazimishwa kulea watoto ambao sio wao.

Kwa hivyo, mandhari hayo ya nyumbani na mjini yamesaidia mwandishi kufanikisha ujumbe wa utabaka. Mwandishi ametumia mandhari hayo kuonyesha tofauti ya maisha katika matabaka hayo mawili. Pia amedhihirisha vile tabaka la matajiri linadhulumu tabaka la maskini.

## 4.5 UHALISIA WA MANDHARI

### 4.5.1 Utangulizi

Sura hii tunatathimini uhalisia wa mandhari yaliyotumiwa na waandishi na kubaini iwapo yametoa picha halisi za hali ya jamii. Mandhari ni mahali maalum palipojengwa na mwandishi mnamotukia matukio mbalimbali katika kazi ya fasihi. Kwa kawaida mandhari huwa ya hali halisi au mandhari ya kubuni. Waandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika* wametumia mandhari yanayoakisi hali halisi za jamii. Mandhari yaliyotumika yanadhihirika katika jamii. Baadhi ya mandhari yaliyotumika katika riwaya hizi ni mandhari ya mahali, mandhari ya wakati na mandhari ya hali.

### 4.5.2 Uhalisia katika riwaya Maisha Kitendawili na Rosa Mistika

Waandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika* wametumia mandhari yafuatayo kuonyesha hali halisi ya jamii. Kwanza wametumia mandhari ya nyumbani. Kupitia mandhari haya wameonyesha yale mambo ambayo wanajamii wanapitia wakiwa nyumbani mwao. Katika riwaya hizi mbili jamii ya wandishi imegawika katika makundi mawili makuu. Kundi la maskini na kundi la matajiri. Kundi la wenye mali linaonyeshwa kwa kuishi katika mitaa ya kifahari, wanamiliki magari ya kifahari kama Marcedez Benz na Volvo. Pia wanafanyia makutano yao katika hoteli za kifahari ambazo zinatambulika kama Five Star Hotel International na Florida Club. Majumba yao yamejengwa kwa gharama ghali, yanazunguukwa na ua na pia yanalindwa usiku na mchana. Familia za matajiri hawasumbuki kupata chakula. Mandhari haya ni halisi katika jamii ya mhakiki. Wanaishi katika mitaa yao. Kwa mfano katika nchi ya Kenya wanaishi mitaa kama Kileleshwa, Muthaiga na Karen. Pia majengo yao yamejengewa nyua ambazo zinazunguuka nyumba zao. Kila jengo lina walinzi wa mlangoni mchana na usiku. Isitioshe, mikutano yao hufanyika katika hoteli kubwa za kifahari kama Serena Hotel, Hilton, Newfork, Safari club na hoteli nyinginezo jijini Nairobi ambapo bei ya vyakula huwa ghali. Zaidi ya hayo, majumba ya matajiri yamejaa vitu vya thamana kama jokofu, samani za bei ghali, nyumba zao zimegawa katika sehemu mbalimbali kama sebuleni, vyumba vya kupumzika, vyumba vya kulala pamoja na vya wageni. Pia vingine vina sehemu ya kubarizi. Hii ni ishara ya kuwa familia hizo ni tajiri.

Kundi la wasio na mali katika riwaya linaonyeshwa kwa kuishi katika nyumba ambazo zimejengwa kwa udongo. Nyumba hizi zinapatikana katika mitaa ya mabanda. Mfano mitaa ya Mathare, Kibra, Mukuru kwa Njenga, Pipeline jijini Nairobi. Katika mandhari

haya chakula kupatikana ni shida, wizi ni jambo la kawaida. Pia watoto katika mandhari haya wanachezea mahali kuna mrundiko wa uchafu. Kazi ambazo wanafanya wanaoishi katika mazingira haya hazina mapato mazuri, mfano kuuza makaa na pombe ya chang'aa. Watoto wanavaa mavazi yaliyoraruka. Mandhari haya ni halisi katika nchi za Afrika ambazo hazijaendelea na ambazo zinakumbwa na changamoto za kiuchumi na uongozi mbaya. Mandhari haya ya mabanda yanadhihirika kwa kuwa na mazingira ambayo hayavutii kamwe. Mandhari haya huonyesha shida ambazo wanajamii hupitia kila siku.

Mandhari ya Shuleni. Wandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wametumia mandhari ya shuleni kuonyesha umuhimu wa elimu, udhibiti wa vijana na uozo katika taasisi za elimu. Mandhari ya taasisi za elimu yametumiwa kuonyesha uhalisia katika taasisi hizo. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*, mwandishi ametumia mandhari ya Chuo cha Mzalendo kuonyesha mambo kadhaa yanayotukia. Kwanza mwandishi anaonyesha kuwa kuna wanafunzi ambao wanathamini masomo kama Rose, Farida na Juma ambao wanasoma hadi wanafuzu. Mwandishi anaonyesha vile wazazi wa wanaofuzu walihudhuria sherehe ya kufuzu kwao. Jambo hili linadhihirisha jamii ya mwandishi ilithamini elimu. Sherehe mbalimbali huandaliwa na vyuo mbalimbali vikuu na vya kiufundi. Wazazi, marafiki na wanajamii huhudhuria sherehe hizi kwa ajili ya kufurahia pamoja na wanaofuzu. Jambo hili linadhihirisha kuwa elimu ni muhimu katika jamii.

Pia baada ya kufuzu mahafali wanapewa vyeti vyao. Vyeti hivi ndivyo wanavyotumia kutafuta kazi. Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anatumia mhuska Rosa kuonyesha kuwa baada ya kupata mafunzo katika Chuo cha Ualimu cha Morogoro anatunukiwa cheti ambacho anakitumia kutafuta kazi. Vivyo hivyo katika jamii, sherehe za kufuzu huandaliwa na pia wanaofuzu wanapewa vyeti vyao kwa ajili ya kutafuta kazi.

Katika vyuo vya Ualimu kama Chuo cha Ualimu cha Machakos, Shanzu, Kamwenja, Bondo, Asumbi na vinginevyo nchini Kenya.

Mandhari ya shuleni pia yanadhihirisha jinsi wanafunzi wanadhibitiwa shuleni. Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* ameonyesha jinsi wanafunzi walidhibitiwa katika shule ya Rosary. Sheria kali ziliwekwa na pia shule zenyewe zilizunguukwa na nyua ambazo ziliwazuia wanafunzi kutoroka shuleni. Jambo hili linadhihirika katika jamii, kila shule imeweka sheria ambazo zinafuatwa na kila mwanafunzi. Sheria hizi huwadhibiti wanafunzi shuleni. Pia shule nyingi katika jamii zimejengewa nyua au nyingine zimepandwa maua ambayo yanawadhibiti wanafunzi shuleni. Isitoshe kila shule huwa na lango kuu ambapo huwa na mlinzi. Mfano shule ya wasichana ya Machakos, Alliance, Kenya High, Pangani na nyinginezo hapa nchini Kenya. Jambo hili huhakikisha kuwa usalama wa wanafunzi na pia wanafunzi wanadhibitiwa shuleni.

Waandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wametumia mandhari ya shuleni kuonyesha udanganyifu katika mitihani shuleni. Katika *Maisha Kitendawili* mwandishi anadhihirisha kuwa kuna wale ambao wanatumia njia za udanganyifu katika kupita mitihani yao. Kuna wale ambao wanaiba mitihani kwa kuandika sehemu mbalimbali za mwili au kwenye karatasi. Pia kuna wale ambao hufanya urafiki na wale wahadhiri na kuhakikisha kuwa hawafeli mtihani. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi anadokeza kuwa mhusika Rosa alifanya mapenzi na Bwana Thomas ambaye alikuwa mkuu wa chuo na kuahidiwa kuwa lazima atapata cheti cha kufuzu. Mambo yaya haya ya kuiba mitihani na kutumia njia za udanganyifu ni halisi shuleni na vyuo mbalimbali katika jamii ya mhakiki. Mfano, Gazeti La Taifa Leo, Desemba tarehe 22, 2018, waziri wa elimu nchini Kenya alitangaza kuwa wanafunzi 1,250 katika shule kumi hawatapata matokeo kwa

sababu ya visa vya udanganyifu. Udanganyifu huo ulitokea kupitia kwa wanafunzi kufanyiwa mtihani, wanafunzi kupata karatasi za mtihani kabla ya muda rasmi wa kuanza mtihani na wengine kupatikana na vifaa vya eletroniki katika chumba cha mtihani.

Mandhari ya Hospitali. Mwandishi ametumia mandhari ya hospitali kuonyesha mateso yanayopitiwa na wagonjwa hospitalini. Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametoa picha halisi ya mateso wanayokumbana nayo wagonjwa pindi wanapotafuta matibabu hospitalini. Kwanza utawala wa hospitali unakosa kuwajibika. Hii ni kupitia mhusika Omar ambapo tunapata picha ya vile mandhari hayo ya hospitali yalikuwa. Sakafu ilikuwa chafu, pia wahudumu wa hospitali wanafika kazini kuchelewa na pia hospitali kukosa dawa. Zaidi ya hayo, wahudumu wa hospitali baadhi yao wanakosa uadilifu. Baadhi ya madaktari na wauguzi wanapuuza wagonjwa ambao wamezidiwa na ugonjwa. Mwandishi anatudokezea kuwa mgonjwa aliyetembelea hospitali akiwa amezidiwa anafariki kwa sababu ya mapuuza ya madaktari.

Mandhari haya ya hospitali ni halisi. Yametoa picha halisi ya mateso ambayo yanapitiwa na wagonjwa katika hospitali za umma. Mfano, pindi tu mfumo wa Ugatuzi ulipoanza kutumika hapa nchini Kenya, wizara ya afya ilikuwa mojawapo ya wizara iliyopewa usimamizi wa kaunti. Kaunti mbalimbali zimekubwa na changamoto nyingi katika usimamizi wa wizara hii. Kila mara tumeshuhudia migomo ya wauguzi na madaktari wakidai kutolipwa mishahara yao. Pia wagonjwa wanapotembelea hospitali hizi wanapata hakuna dawa na kulazimika kununua katika maduka ya kibinafsi. Pia hospitali hizi kunashuhudiwa umati wa watu ambao wamefika kwa ajili ya kupata matibabu. Umati huu unaanza kuhudumiwa kwa kuchelewa sana, pia wakati mwingine wanaanza kuhudumiwa baada ya tukio la kifo cha mgonjwa. Zaidi ya hayo, baadhi ya hospitali hakuna vitanda vya

kutosha vya wagonjwa. Pia baadhi ya madaktari wanafika hospitali kwa muda mfupi kisha wanaondoka hospitalini kwenda kufanya shughuli zao. Mfano, Gazeti la Daily Nation Septemba tarehe 13, 2022 kuliripotiwa kisa cha mtoto aliyefariki katika hospitali kuu ya Kenyatta kutokana na upuuzaji wa madaktari. Mamake mtoto huyo alisema kuwa baada ya kufika hospitalini, wasimamizi wa hospitali walidai hakuna vitanda vya kutosha na pia alistahili kulipa kabla ya kuhudumiwa. Familia hii ilikesha katika chumba cha wagonjwa mahututi bila kupata huduma yoyote. Mtoto huyo alifariki kabla ya kupelekwa katika chumba cha upasuaji. Jambo hili linaashiria kutowajibika kwao katika kazi zao.

Mandhari ya Kanisani. Mwandishi ametumia mandhari ya kanisani ili kupitisha ujumbe wa unafiki wa kidini na upujaji wa waumini na viongozi wa kidini. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* mwandishi ametumia mhusika Rose kudhihirisha waumini wanafiki. Mwandishi anatudokezea kuwa mhusika Rose alitenda mambo ambayo yalikuwa kinyume na kanuni za Mungu, ila kila siku ya Jumapili ndiye anayeongoza kwa nyimbo na pia kukemea matendo maovu kanisani. Zaidi ya hayo, mwandishi ametumia kanisa la Msalaba Mweusi kuonyesha unafiki wa kiongozi wa kidini. Mandhari ya kanisa hili yalikuwa ya kuogofya ila kanisa hili lilijaa waumini waliotaka kuombewa. Jambo hili linadhihirisha utapeli katika majumba ya kuabudu. Mandhari haya ni halisi kwa kuwa mambo wanayozungumziwa yanadhihirika katika jamii ya mhakiki. Kanisa limetumika kama mahali pa maficho baada ya waumini kutenda maovu. Viongozi wa kanisa baadhi yao wamebadilisha kanisa na kuwa sehemu ya kupata utajiri. Waumini wanapujwa kwa kudanganywa na kutapeliwa pesa zao kwa madai wanaombewa. Pia viongozi wa kanisa wanatafuta njia mbalimbali za kutwaa mamlaka na pia nguvu zisizo za kawaida za kushawishi waumini.

Mandhari ya Mazishini. Waandishi wa riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wametumia mandhari ya mazishi kuonyesha hali mbalimbali wanazopitia wanajamii. Pia mandhari haya yametoa picha halisi ya mila na taratibu zinazofutwa na wanajamii. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi ameonyesha mila ambazo zinafuatwa wakati wa mazishi. Mila hizo ni kama familia ya marehemu wakati wa maziko kukaa karibu na jeneza. Pia baada ya kaburi kuwa tayari, maiti huoshwa. Zaidi ya hayo wanaofika wakati wa mazishi wanapewa fursa ya kuutazama uso wa marehemu kwa ajili ya kumpa heshima ya mwisho. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* mila na taratibu hufuatwa wakati wa maombolezo na pia wakati wa mazishi. Taratibu hizi zinadhihirika wakati wa mazishi ya Omar na Kibibi. Kwanza jambo hili lilidhihirisha ushirikiano wa jamii wakati wa mazishi. Pia mwandishi anatudokezea kuwa siku ya mazishi huwa kuna utaratibu ambao unafuatwa. Si kila mtu hupewa ruhusa ya kuzungumza kwenye mazishi.

Mandhari hayo ya mazishi ni halisi katika jamii ya mhakiki. Taratibu zote zinazofuatwa na jamii ya mwandishi wakati wa mazishi zinafuatwa katika jamii ya msomaji. Wanajamii wanapewa fursa ya kumpa heshima ya mwisho marehemu kwa kuutazama uso wake. Pia familia ya marehemu hukaa karibu na jeneza. Pia kuna utaratibu unaofuatwa katika siku ya mazishi. Utaratibu huo unafuatwa ili shughuli kuendelea jinsi inavyostahili.

Mandhari ya Ugangani. Waandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wametumia mandhari haya kuonyesha hali ambazo wanajamii hupitia kwa kudanganywa na waganga. Hali hizi ngumu zinaweza kuwa za ugonjwa, matatizo ya familia na kupoteza mali kupitia wizi. Picha ambazo wandishi wametoa kuhusu mandhari ya kwa mganga yanadhihirika katika hali halisi ya jamii. Mandhari haya huchorwa yakiwa yamepangwa kwa namna fulani. Vibuyu kuning'inia mlangoni, nyumba kujengwa tofauti na nyumba

zingine na mganga kuvaa mavazi yaliyotofauti na ya watu wengine wa kawaida. Jambo hili huwapa imani watu kuwa waganga hawa wana uwezo wa kutatua shida wanazopitia. Kupitia imani hii wanajamii wanatapeliwa mali yao.

Mandhari haya ya ugangani ni halisi kwani yanadhihirika katika jamii ya mhakiki. Mabango mbalimbali yamewekwa katika barabara mbalimbali za miji yakitangaza mambo ambayo waganga wanayatatua. Isitoshe, kwenye mabango hayo nambari zao za simu huandikwa kwa ajili ya kuwasiliana nao. Mambo haya katika nadharia ya uhalisia, yanadhihirisha uhalisia wa mambo yanayofanyika katika jamii na uhalisia wake. Katika jamii suala la imani potofu linaonekana waziwazi pale watu wanapougua hukimbilia kwa waganga wa jadi badala ya kwenda hospitali kupata matibabu. Vyombo vya habari vya nchi za Afrika Mashariki kila mara hutangaza kuwa watu mbalimbali walitapeliwa mali yao baada ya kutafuta usaidizi kwa waganga.

**4.6 Hitimisho**

Katika sura hii tumechunguza mandhari mbalimbali na kuainisha katika makundi matatu ambayo ni mandhari ya mahali, mandhari ya wakati na mandhari ya hali. Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia mandhari halisi ambayo yanaonekana katika mazingira halisi ili kuwasilisha ujumbe wake. Mandhari hayo ni kama: mandhari ya nyumbani, mandhari ya chuoni, mandhari ya kanisani, mandhari ya mjini, hospitalini na mandhari ya mazishini.

Mandhari haya yametumika kuwasilisha ujumbe ufuatao. Mandhari ya nyumbani yametumika kuwasilisha ujumbe wa utabaka unaodhihirika katika jamii. Utabaka huu unadhihirika kupitia makundi mawili, tabaka la juu (matajiri), ambalo linaonyesha watu ambao wanamiliki magari ya kifahari, majumba ya kukodisha, wamejenga nyumba za bei

ghali na wanaishi maisha ya starehe katika jamii na tabaka la chini (maskini), ambalo linaonyesha wale hawana magari, hawana majumba ya kukodisha, wanaishi katika miji ya mabanda, kupata chakula ni tabu na wanapitia changamoto nyingi za maisha.

Mandhari mengine yaliyodhihirika ni ya chuoni. Mandhari haya yametumika kufanikisha ujumbe wa thamani ya elimu katika jamii. Hili linashuhudiwa kupitia kufuzu kwa wanafunzi mbalimbali katika jamii na jinsi jamii ilihakikisha watoto wamepata elimu bila kubagua. Pia mandhari haya yamewasilisha uozo unaotendeka katika vyuo mbalimbali kama udanganyifu wa mitihani na ufisadi unaoendelezwa katika idara mbalimbali za elimu.

Mandhari ya kanisani yametumika kufanikisha ujumbe wa unafiki unaoendeshwa na viongozi wa kanisa na pia waumini. Kanisa limetumika kama maficho kwa wanaotenda maovu. Pia viongozi wa kanisa wamelibadilisha kanisa na kuwa chumba cha biashara badala ya kuhubiri neno la Mungu. Mwandishi ametumia mandhari ya hospitali kuwasilisha mateso yanayowapata wagonjwa kwa sababu ya kutowajibika kwa utawala wa hospitali na pia wahudumu wa hospitali kukosa uadilifu katika kazi zao.

Zaidi ya hayo mwandishi ametumia mandhari ya ugangani kudhihirisha swala la ushirikina na ulaghai unaotendeka katika jamii. Kupitia mandhari haya mwandishi anadhihirisha jinsi wanajamii wanatapeliwa na kulaghaiwa mali yao baada ya kutafuta huduma kwa waganga. Mwandishi ametumia mandhari ya mazishini kuonyesha mila na tamaduni ambazo zinadumishwa na jamii ya mwandishi. Pia mandhari haya yametumika kuonyesha mateso wanayoyapitia mayatima baada ya wazazi wao kufariki.

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* ametumia mandhari yafuatayo. Kwanza mandhari ya nyumbani. Kupitia mandhari haya tunapata ujumbe wa utabaka, uvumilivu katika ndoa

na dhuluma ambazo ziliendeshwa katika jamii ya mwandishi. Dhuluma hizi ni kama kupigwa kwa wanawake na bwana zao na udhibiti wa kupindukia wa mabinti kutoka kwa baba zao.

Mandhari mengine yaliyotumika ni mandhari ya shuleni. Mwandishi ametumia mandhari haya kufanikisha ujumbe wa udhibiti wa vijana shuleni. Hili linadhihirika katika shule ya msingi na shule ya upili. Isitoshe, mwandishi ametumia mandhari haya kuonyesha kuwa baada ya wanafunzi kujiuga na vyuo jambo la udhibiti halizingatiwi. Pia mandhari haya ya shuleni yametumiwa kuwasilisha uozo unaotendeka shuleni na vyuoni kupitia kwa wanafunzi na wahadhiri.

Mandhari ya baa ni mandhari yaliyotumika na mwandishi kwa ajili ya kufichua uozo unaotendeka katika jamii. Mandhari haya yametumika kudhihirisha uozo unaotendeka katika sehemu ya kunywea pombe. Mwandishi anadhihirisha jinsi wanajamii wamepotoka kimaadili na kutumia mandhari haya kama njia ya kupora wengine.

Zaidi ya hayo, mwandishi ametumia mandhari ya usiku. Mandhari haya yametumika kuonyesha yale mambo ambayo hutendeka usiku. Kupitia mandhari haya mwandishi anaonyesha jinsi wahusika walitenda mambo kinyume na maadili ya jamii hiyo wakati wa usiku. Kwanza kupitia mhusika Zakaria tunapata anamdhulumu binti yake usiku kwa kumpiga. Pia mhusika Rosa anafanya uzinzi na mkuu wa chuo usiku. Mandhari haya pia yametumiwa kufanikisha swala la utabaka katika jamii.

Katika sehemu hii tumebainisha mchango wa mandhari katika riwaya teule. Tumeona ni vipi mandhari yanavyochangia kufanikisha ujumbe wa wandishi katika riwaya teule. Wandishi wa riwaya *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika* wametumia mandhari

mbalimbali kufanikisha ujumbe waliokusudia. Katika riwaya ya Maisha Kitendawili tumebainisha ujumbe wa mwandishi kama: utabaka, dhuluma zinazoendelezwa kwenye jamii, kudumishwa kwa tamaduni na uvumilivu katika ndoa. Ujumbe huu wa mwandishi umefanikishwa kupitia mandhari yafuatayo; mandhari ya mjini, nyumbani, hospitalini, kanisani, kazini na mazishini.

Ujumbe tuliobainisha katika riwaya ya Rosa Mistika ni kama: uvumilivu katika ndoa, nafasi ya mwanamke katika jamii ya mwandishi, dhuluma zinazoshuhudiwa, tamadumi zinazodumishwa katika jamii na tabaka mbalimbali. Ujumbe huu umedhihirika kupitia mandhari yafuatayo; mandhari ya hospitalini, chuoni, nyumbani, klabuni, kijijini, mazishini na mandhari ya usiku. Mchango wa mandhari katika riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika* umedhihirika bayana katika kufanikisha ujumbe wa waandishi.

Pia tumetathmini mandhari mbalimbali yaliyotumiwa na waandishi iwapo yameakisi hali halisi ya jamii. Wandishi wa riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wametumia mandhari ambayo yanadhihirika katika jamii na yanawasilisha ujumbe unaodhihirika katika jamii halisi. Mandhari hayo ni mandhari ya nyumbani ambayo yanatoa picha halisi ya yale yanayopatikana nyumbani na jinsi jamii zimejigawa kulingana na uwezo wao wa kimapato. Wandishi hao wameonyesha mandhari ya matabaka mawili ya jamii yao. Matabaka haya pia yanadhihirika katika jamii halisi ya mhakiki.

Mandhari ya shuleni pia yametumika katika riwaya zote mbili. Waandishi wa riwaya hizi wameonyesha jinsi shughuli mbalimbali zilivyoendeshwa katika taasisi za elimu. Taasisi hizi za elimu zilikuwa na sheria ambazo zilitumika kudhibiti wanafunzi wao. Sheria hizi

zilidhibiti wanafunzi hadi shule za sekondari. Baada ya wanafunzi kujiunga na vyuo udhibiti huu hautiliwi maanani. Vivyo hivyo ndivyo hali ilivyo katika shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu. Pia mandhari hayo ya shule yamefichua jinsi jamii za wandishi zilivyodhamini elimu kwa kuhakikisha kila jinsia imepata elimu. Katika jamii halisi hasa nchini Kenya kila mtu anazingatia elimu kwa jinsia zote. Serikali imehakikisha kila jinsia imepata elimu kwa usawa.

Waandishi wa riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wametumia mandhari ya hospitali. Mandhari hayo yametumika kudhihirisha mateso wanayopitia wagonjwa wanapotafuta matibabu. Mateso haya ni kama ukosefu wa dawa, kutowajibika kwa utawala wa hospitali na ukosefu wa maadili wa wauguzi na madaktari. Changamoto hizi za ukosefu wa dawa, ukosefu wa vitanda vya wagonjwa na ukosefu wa maadili ya madktari na wauguzi zinadhihirika katika hospitali halisi. Hospitali nyingi za umma hapa nchini Kenya zinapitia changamoto sawia.

Mandhari ya kanisani pia yametumika na waandishi wote wawili. Wandishi hawa wametoa picha halisi ya mambo ambayo yanatendeka katika jamii yao. Mandhari haya yamefichua uozo unaoendelezwa na waumini na viongozi wa kanisa. Uozo huu ni kama utapeli na unafiki wa waumini pamoja na viongozi wa kanisa. Maswala hayo ya unafiki na utapeli unadhihirika katika jamii halisi. Kanisa limebadilishwa kuwa nyumba ya biashara badala ya kuwa nyumba ya kufanyia maombi. Mambo haya ya unafiki na utapeli kila mara yanadhihirika katika bara la Afrika. Viongozi kanisani wanapigania uongozi, makanisa yanafanya shughuli za kutapeli waumini kwa madai kuwa wanawauzia mafuta na pia viongozi wa kanisani kufumaniwa wakifanya vitendo ambavyo ni kinyume na kanuni za dini zao.

# SURA YA TANO
# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia muhtasari wa utafiti wetu kutoka sura ya kwanza hadi ya nne. Pia tumetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu. Matokeo haya yameongozwa na madhumuni ya utafiti wetu kwa kuzingatia nadharia ya uhalisia. Yale yaliyobainika kutokana na uchanganuzi wa mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi yameshughulikiwa. Pia mapendekezo yametolewa kwa ajili ya watafiti wengine.

Utafiti huu umechunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Tumejadili aina mbalimbali za mandhari yaliyotumika na wandishi katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. Pia tumebainisha mchango wa mandhari hayo katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Hatimaye tumetathmini iwapo mandhari yaliyotumiwa na waandishi yameakisi hali halisi ya jamii. Madhumuni haya ya utafiti yamechanganuliwa na kuelezwa kwa kuzingatia nadharia ya uhalisia.

## 5.1 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa wandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Pia utafiti huu ulilenga kuyatimiza malengo matatu. Lengo la kwanza ni kubainisha aina ya mandhari yaliyotumiwa na wandishi wa *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*. Utafiti huu umetambua kuwa waandishi hawa walitumia mandhari ya aina mbalimbali. Mandhari ambayo yamepatikana katika riwaya hizi ni mandhari ya mahali, mandhari ya wakati na mandhri ya hali.

Mandhari ya mahali yametumika kuelezea ni wapi tukio limetendeka katika riwaya. Mandhari ya mahali ambayo yamedhihirika katika riwaya ni mandhari ya chuoni, mandhari ya mjini, mandhari ya hospitalini, mandhari ya baa, mandhari ya kanisani na mandhari ya ugangani. Mandhari ya hali yamedhihirika kupitia hali ambazo jamii za wandishi zilipitia. Mandhari ya hali ni pamoja na mandhari ya mazishini na mandhari ya uvumilivu. Aina ya tatu ya mandhari ni ya wakati. Mandhari haya yametumika kuonyesha ni lini jambo lilitokea. Wandishi hawa wametumia mandhari ya wakati wa usiku ili kuonyesha vitendo vilivyotendwa wakati wa usiku katika jamii ya wandishi.

Lengo la pili katika utafiti huu lilikuwa kuchunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa wandishi. Lengo hili lilidhamiria kujibu swali la: mandhari yana umuhimu gani katika riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*? Baada ya kuchunguza kipengele cha mandhari tumebaini kuwa waandishi wa riwaya hizi wametumia kipengele hiki katika kujenga na kuwasilisha ujumbe wao. Hii ni kwa sababu baada ya kuchunguza aina tatu ya mandhari yaliyotumika na waandishi, tumepata kuwa ujumbe unaofanikishwa na mandhari hayo ni utabaka, dhuluma zinazodhihirika katika jamii za waandishi, uvumilivu katika ndoa, utamaduni wa jamii ya wandishi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Kila mandhari yaliambatana na ujumbe kwenye hadithi za wandishi. Mfano katika mandhari ya hospitalini wandishi wametoa taswira halisi ya jinsi wagonjwa wanapitia mateso wanapotafuta matibabu. Mateso hayo ni: kufika hospitali na kupata wahudumu bado kufika hospitalini, ukosefu wa dawa katika hospitali na mandhari ya hospitali kuwa chafu.

Lengo la tatu la utafiti lilikuwa kutathmini iwapo mandhari yaliyotumiwa na waandishi yameakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Suala la utabaka ni uhalisia unaojitokeza katika

riwaya *MaishaKitendawili* ambako mwandishi ametumia wahusika Kasu na Yasmini wakiwa katika mandhari ya mjini hasa mjini Soweto. Mwandishi anaelezea shida ambazo walioishi mjini Soweto walipitia. Hivyo, kutokana na nadharia ya uhalisia mwandishi ametumia mandhari halisi ambayo yanadhihirika katika jamii zetu. Malengo ya utafiti yameweza kufikiwa. Ni matumaini kuwa tumetoa mchango wa kutegemewa katika kuelewa umuhimu wa mandhari katika riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*.

## 5. 2 Hitimisho

Katika kazi hii tulidhamiria kuchunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa wandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*. Katika utafiti huu tumebainisha kuwa kipengele cha mandhari kina mchango mkubwa katika kudhibiti ujumbe. Mandhari husaidia mwandishi kuchora taswira ya yale yanayotendeka katika jamii na kumwezesha mwandishi kufanikisha ujumbe wake. Kwa hivyo, bila mandhari ingekuwa vigumu kwa waandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika* kuwasilisha ujumbe unaoleweka kwa urahisi. Pia wandishi Euphrase Kezilahabi na John Habwe wamefanikiwa katika kutumia kipengele cha mandhari kufanikisha ujumbe wao. Waandishi hawa wametumia mandhari kwa usawa. Hii ni kwa sababu mandhari yaliyodhihirika katika riwaya ya *RosaMistika* pia yanadhihirika katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Mandhari hayo ni pamoja na mandhari ya nyumbani, chuoni, kanisani, baa, mjini, mazishini, ugangani, hospitalini na mandhari ya usiku. Mandhari haya ni halisi na yanadhihirika katika karne ya ishirini na moja. Utofauti uliopo katika mandhari ya riwaya ya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* unatokana na kubadilika kwa miundo msingi na mabadiliko ya njia za kiuchumi, ila mandhari ni yayo hayo.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia hii husisitiza kuwa kazi ya mwandishi inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Waandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika* wametumia mandhari halisi kudhihirisha mambo halisi yanayodhihirika katika jamii ya sasa.

### 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na manufaa kwa wasomi wa fasihi ya Kiswahili, wahakiki, wanafunzi wa vyuo vikuu, walimu na wakuza mitaala. Vilevile matokeo ya utafiti huu yatachangia katika taaluma ya uhakiki na fasihi ya Kiswahili kwa jumla. Waandishi wa riwaya wataona uhusiano wa mandhari na ujumbe katika kufanikisha kazi zao.

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umeshughulikia mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya. Kwa kuwa tunaamini kuwa hakuna utafiti unaoweza kukamilisha kila jambo, tunapendekeza yafuatayo: kwanza utafiti ufanywe kuhusu mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe katika tanzu nyingine za fasihi kama tamthilia na hadithi fupi. Pia katika utafiti huu tumetumia nadharia ya uhalisia kuyabainisha masuala yanayoibuka katika jamii. Tunapendekeza utafiti mwingine kufanywa kuhusu mchango wa mandhari kwa kutumia nadharia nyingine kama uamilifu. Mwisho tunapendekeza utafiti ufanywe kuhusu namna mandhari yanavyoathiri wahusika.

## MAREJELEO


Allan H.G. (1962). *Literary Criticism. Plato to Dryden*. Detroit: Wayne State University Press.

Arron, H. (1977). *Marxist Aesthetics*. Cornell University Press, London.

*Encyclopaedia Britannica Volume 9.*

*Daily Nation*, September 13, 2022 "A Mother's Agony and Child's Slow Painful Death." uk. 2

*Daily Nation*, December 22, 2018 "Knec Cancels Results of Candidates." uk.3

Donna, E.N. (1992). *The Impact of Literature Based Reading*. Upper Saddle: Pearson Education.

Habwe, J. (2000). *Maisha Kitendawili*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Jameson, F. (1981). *The Political Unconscious: Narrative as a Socially Symbolic act*. London: Methuen.

JKF (2016). Kamusi Elezi ya Kiswahili. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kamunde, M.E. (1983). "Kilio cha Wanyonge; katika Riwaya za Said Ahmed Mohammed". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Katola, E (2006). "Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike Tamthilia za Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Khaemba, S.S. (1999). "Ulinganishi wa Maudhui ya Mapinduzi katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru*", Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kothari, C. R. (2004*). Research Methodology; Methods and Technique*, New Delhi: Wishwa Prakashan.

Kweyu, D.A. (2007). "A Critical Analysis of Patriarchy and Masculinity in Kezilahabi's

*Rosa Mistika* and *KichwaMaji*". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Lodge, D. (1972). *20th Century Literary Critism*. London. Longman.

Lucaks, G. (1972). *The Meaning of Contemporary Realism*. Londan: Merlin Press.

Lugano, C. (1989). "Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Massamba, D. (2009). *Kamusi ya Isimu na Lugha, Falsafa ya Lugha*. Dares Salaam. TUKI,

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishers.

________ (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo yake*; Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mbiti J.S (2014) *African Religions and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S.A. (1995). *Riwaya, Tamthilia na Hadithi fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Moser. C. (1993) *Gender Planning and Development. Theory, Practice and Training*. Routledge: London.

Mugenda, O. and Mugenda, A. (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches,* Nairobi: Act Press.

Muusya, J.K. (2012). "Mandhari katika hadithi fupi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika makahaba katika riwaya za S.A Mohammed". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mwenda, N. (2004). *Uhakiki wa kazi ya Fasihi*. Rock Island: Augustana College, U.S.A.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. and Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Kenya. Jomo Kenyatta Foundation.

Nkoge, G. (2006). "Athari za Udhanaishi katika *Kichwa Maji* na *Nguvu ya Sala*." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nyoasi, K. (2008). "Taswira ya Asasi ya Ndoa katika Riwaya za *Kiu* na *Msimu wa Vipepeo*." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Obure, E.M. (2012). "Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike Katika Riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini*". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Omar, R. Z. (2011) "Athari za Lugha ya Utani katika Jamii ya Wapemba, Zanzibar." Tasnifu ya Uamili, Chuo Kikuu cha Uganda. (Haijachapishwa).

Sengo, T. Y. na Lucas, S. (1975) *Utani na Jamii Ukwere,* Nairobi: Foundation Books L.t.d

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dares Salaam: Press and Publishing Centre.

*Taifa leo*, Agosti 3- 2018. "Dhuluma katika ndoa"uk. 5

Tambasi, P. (2011). "Uhakiki wa Fani katika Utenzi wa Tambuka." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

The Bible Societies (1971). *The Holy Bible*. New York: Collins Bible.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa fasihi*: *Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

______ (2003) *Kamusi ya fasihi, Istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

______(2008) *Misingi ya Uchambuzi wa fasihi*. Nairobi. Vide Mulwa Publishers Ltd.

Quraishy, M.A (1989). *Textbook of Islam Book2.* Nairobi: The Islamic Foundation.

**KIAMBATISHO I**

# MACHAKOS UNIVERSITY
## OFFICE OF THE DEAN GRADUATE SCHOOL

Telephone:254-(0)735247939, (0)723805929
Email: graduateschool@mksu.ac.ke
Website: www.machakosuniversity.ac.ke

P.O Box 136-90100
Machakos
**KENYA**

REF. MksU/GS/SS/011/VOL.1

7th July, 2022

The Director,
National Commission for Science, Technology and Innovation,
P.O Box 30623,
**NAIROBI.**

Dear Sir,

**RE: SHADRACK TETE MUIA (C50/7325/2016)**

The above named is a Masters student in the second year of study and has cleared course work. The University has cleared him to conduct a research entitled: **"Mchango wa Mandhari katika Kufanikisha Ujumbe wa Mwandishi."**

Kindly assist him with a Research Permit in order to undertake the research.

Thank you.

**PROF. KIMITI RICHARD PETER, PhD**
**DEAN GRADUATE SCHOOL**

KRP/gm

ISO 9001:2015 Certified ……………………………*Soaring Heights in Transforming Industry and Economy*

## KIAMBATISHO II



REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 530553

Date of Issue: 21/July/2022

**RESEARCH LICENSE**

**This is to Certify that Mr.. SHADRACK TETE MUIA of Machakos University, has been licensed to conduct research in Machakos on the topic: MCHANGO WA MANDHARI KATIKA KUFANIKISA UJUMBE WA MWANDISHI for the period ending : 21/July/2023.**

License No: NACOSTI/P/22/18954

530553

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.